

BARTIMAYO KIPOFU

 ...?...Mwaweza kuketi, tafadhalini. Nimeona watu wengi wakituma haja, na, kwa ajili ya maombi. Sasa, hiyo ni... Tunathamini hilo sana, kwa sababu hiyo Biblia ilisema ya kwamba walichukua kutoka katika mwili wa Paulo, lesa na nguo, na pepo wachafu wakawatoka watu, na ugonjwa mbaya ukawaacha, na maradhi. Naye Mungu angali ni Mungu, Yeye yuko leo tu kama alivyokuwa katika siku za—za Mtakatifu Paulo, Yeye kamwe habadiliki.

² Sasa, watu wengi huchukua vitambaa hivyo na kuvipaka mafuta, na kuwapelekea wapendwa, sasa, hilo—hilo ni sawa kabisa. Chochote Mungu anachobariki, na—nakiunga mkono moja kwa moja, sivyo na nyinyi? Naam. Lakini, Kimaandiko, Paulo hakuzipaka mafuta, walizitoa mwilini mwake, Matendo 19 ilisema walitoa mwilini mwake, nao pe—pepo wachafu wakawaacha watu.

³ Sasa, mimi...Tunajua ya kwamba—ya kwamba Mtakatifu Paulo, sisi si Mtakatifu Paulo, lakini Yeye angali ni Yesu. Kwa hiyo basi, Yeye ni Yesu tu usiku wa leo, kama alivyokuwa katika siku za Mtakatifu Paulo. Kwa hiyo, Yeye aliheshimu tu imani ya watu katika mtumishi Wake, Naye atafanya vivyo hivyo kwa ajili yako. Miujiza mikubwa kuliko yote niliyopata kujua imefanywa, ilikuwa ni wakati watu walipotuma vitambaa vidogo vya maombi, ama tulipowatumia, nao wakaonywa, hutuma maelfu ya hivyo, kila juma, kote ulimwenguni.

⁴ Nami nakumbuka huko Afrika Kusini, ambako tulikuwa na mkutano mkubwa kwenye uwanja mkubwa wa ndege, walikuwa wame—wameturuhusu tuuchukue kwa ajili ya mikutano. Hao watu, ilikuwa ni kule Cape Town, kulikuwa na wengi sana, hatukuwa na jengo la kuwaweka ndani, tuliifanyia huko nje kwenye uwanja wa ndege.

⁵ Basi kulikuwa na ninii...Nafikiri yalikuwa, yalikuwa karibu, ninasahau ni magunia mangapi ya haya magunia makubwa ya turubai yaliyojaa barua, na, za kuombewa, nami nikaendelea kuombea barua hizi. Ndipo mmoja wa waandishi wa habari akasema, “Ndugu Branham ni mshirikina sana,” kasema, “alikuwa akiombea barua kuwapelekea wagonjwa.”

⁶ Vema, mnaona, hu—huyo ndugu kamwe hakuelewa kwamba hilo ni agizo la Kimaandiko ambalo tumeachiwa, kwamba tunapaswa kuviombea vitu hivyo.

⁷ Na mfano mdogo tu wake, maana tunataka, usiku wa leo ndio, ama, tumetoa ibada, hasa, usiku wa leo kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa. Kulikuwa na, wakati fulani uliopita, nilikuwa nikisoma moja ya shuhuda zilizorudi, mama mmoja

huko Ujerumani, alikuwa amelemaa kwa yapata miaka kumi na saba, akiketi kwenye kiti cha magurudumu.

⁸ Na wakati ningevituma hivi, tunatuma vipande vidogo vya vitambaa wakati hawavipeleki, maana nilikuwa na uwezo wa kuweka lesa moja ndani, lakini wakati zinakuwa maelfu, nazo lesa ni kama senti kumi na tano, ishirini kila moja, huwezi kufanya hivyo. Na kwa hiyo, tunachukua tu mamia ya yadi za riboni, na kuzikata vipande vidogovidogo, nami ninaombea kila kimoja.

⁹ Iwapo unahitaji moja, agiza tu ofisini, tu—tunaziombea na kuzisambaza, ndipo utakuwa na barua ndogo rasmi. Nao watu huamka saa zote za usiku, wanafanya msururu kote ulimwenguni, maombi kwa ajili ya wagonjwa. Biblia ilisema tungeweza kuungama makosa yetu sisi kwa sisi, na kuombeana. Na kwa hiyo sisi . . . Kote nchini, kote ulimwenguni.

¹⁰ Kwa hiyo maskini mama huyu akapokea yake, na kuna maagizo mle yanayosema, “Kama ukininii . . . Kama inawezekana, mwite mchungaji wako. Halafu basi, kama . . . Acha afanye maombi pamoja nawe unapojivika hii riboni. Na kama mchungaji wako hayuko karibu, basi mwite jirani mwema, Mkristo. Kama umetenda dhambi yoyote, uovu kwa mtu yeyote, umesema uovu, au umefanya jambo lolote baya unalojua, nenda ukarekebishe hilo, kwanza, kabla hujajivika hiyo riboni. Halafu basi, ujiweke tayari, na ndipo wakikufungia huo utepe, basi amini ya kwamba Mungu huponya.”

¹¹ Wauweke, ninawaambia, kwenye vazi lao la ndani karibu na moyo wao. Na baada ya *saa kadhaa*: saa tatu asubuhi, saa sita adhuhuri, na saa tisa alasiri, ulimwenguni kote, kuna msururu wa maombi juu ya jambo hilo. Watu huamka saa nane usiku, na kadhalika, kufanya huo msururu wa maombi kote ulimwenguni. Halafu basi, kama labda watu milioni moja na nusu au milioni mbili wakiombeana kwa wakati mmoja, jambo fulani halina budi kutukia. Mungu, hana budi tu kusikia hayo. Halafu basi, kwa hiyo juu ya hilo, wangeninii . . .

¹² Maskini mama huyu wa Kijerumani, ilikuwa ninii sana, vema, nisingetaka kusema kana kwamba ilikuwa ni kukufuru kulisema, kidogo ni la kupendeza, lakini akasema, “Nilijiwekelea hiyo lesa ndogo.” Akasema, “Huyo hapo mama jirani yangu aliyekuja kuomba pamoja nami,” naye akasema, “Nilikuwa nimeungama dhambi zangu zote, na kumwomba Bwana aniruhusu kutembea tena, ili niweze kumtukuza.” Kasema, “Yote yalipokwisha kufanywa, *Ndugu Branham*,” kasema, “niliweka huo utepe mdogo kwenye vazi langu la ndani, nikasema, ‘Vema, ewe Bw. Ibilisi, ulinishikilia kwa muda mrefu kadiri utakaonishikilia.’” Akainuka kutoka kwenye kiti cha magurudumu, akaenda zake.

13 Rahisi tu hivyo. Kama wewe ukiwa tu rahisi! Mnajua, shida yetu sisi Wakristo, ama, sisi wanadamu tunamfanya Mungu kuwa mbali sana na mgumu sana. Ule urahisi!

14 Nimekuwa nikiona kila usiku baadhi ya Wahindi wameketi papa hapa, hawako hapa, nadhani, usiku wa leo. Lakini mtu fulani aliniambia ya kwamba—ya kwamba kulikuwa na waimbaji waliokuwa wakiimba, wawulana fulani wa Kihindi walikuwa wakiimba, Nnngependa kuwasikia kabla hawajaondoka. Lakini hata hivyo, nilikuwa nikiwazia juu ya mara ya kwanza niliyopata kuwahubiria Wahindi, ilikuwa ni Waapache huko, huko Arizona, huko San Carlos.

15 Na kwa hiyo, Mhindi ni jamaa wa kipekee sana. Niliona hilo baada ya kwenda kuvua samaki hivi majuzi asubuhi, nilimwuliza mtu fulani kile alichokuwa akitumia kama chambo, akasema, “Chambo tu.” Asingeniambia.

Nikasema, “Asante, bwana.” Hakika alikuwa ni mvuvi. Na kwa hiyo, nilikuwa . . . Wao ni wa ajabu sana.

16 Ninakumbuka mvulana wangu wakati mmoja alikuwa akigawa kadi za maombi kwenye mkutano mkubwa wa hema huko Phoenix. Nami nikaona watu wakija kwenye mstari wa maombi wakiwa labda wanaumwa na kichwa, na jino bovu, huku watu wameketi huko nje wakiugua kansa, wakifa.

17 Ndipo nikasema, “Billy, kamwe usifanye hivyo. Waulize hao watu shida waliyo nayo.” Kwa kawaida yeye huchanganya tu kadi na kumpa mtu yeyote anayezitaka. Kwa hiyo basi, nikasema, “Usifanye hivyo.” Nikasema, “Kwa sababu, ukiwauliza hao watu, kuna watu wengi kupita kiasi walio wagonjwa sana hapo kumpa tu jamaa kadi aliye na, anayeumwa na kichwa ama kuumwa na jino, huku mtu ameketi hapo akifa kwa kansa na anataka kuombewa.” Nikasema, “Sasa, hupaswi kufanya hivyo.” Nikasema, “Waulize tu kuna shida gani.”

18 Kwa hiyo Billy anashuka kwenda mkutanoni usiku huo, naye, jamaa mdogo tu wakati huo, naye akachukua kadi zake na kuzichanganya, naye akasema, “Sasa, kila mmoja wenu hana budi kuniambia una shida gani. Baba yangu alisema ya kwamba—ya kwamba nisiwape kadi hizi za maombi watu ambao walikuwa tu wanaumwa na meno, na kuumwa na kichwa, na kadhalika, huku watu wanakufa kwa kansa.”

19 Kwa hiyo, maskini yule chifu, alikuwa ameketi papo hapo sakafuni kama kawaida, naye amevaa kofia yake. Na kwa hiyo, akaenda pale, akaanza kuona kadi za maombi za Billy zikiendelea kupungua zaidi na zaidi alipokuwa akizigawa, akampigapiga begani, akaunyosha mkono wake.

20 Naye akasema, “Chifu,” kasema, “baba yangu alisema ningeninii. . . itakubidi kuniambia shida yako. Kwani wewe ni mgonjwa sana?” Kasema, “Una shida gani?”

Akasema, “Mimi mgonjwa.”

Kwa hiyo akasema, “Vema, nenda ukaketi chini, nawe . . .”

²¹ Akaenda pale na kuanza kuzigawa, ndipo Chifu akaona lile lundo dogo la kadi likipungua zaidi na zaidi, akaja tena, akamgusa mgongoni.

Akasema—akasema, “Kuna shida gani, Chifu?”

Akasema, “Mimi mgonjwa.”

²² Kwa hiyo akasema, “Vema, nitaninii . . . Hebu kidogo.” Na kwa hiyo, alikuwa akisema, “Mtu yeyote aliye mgonjwa sana kwa kansa, ama chochote kile,” kusudi aweze kukupa kadi ya maombi. Baada ya kitambo kidogo, chifu akaona ni mbili ama tatu tu, akakimbia na kumshika Billy.

Akasema, “Mimi mgonjwa.”

Billy akasema, “Chukua kadi hii na uandike juu yake, ‘Mimi mgonjwa,’ kisha uende ukaketi chini.” “Mimi mgonjwa.”

²³ Nika—nikamwona kwenye mstari wa maombi usiku huo, nami nikasema, “Chifu,” nikasema, “Je, . . . ? Unamwamini Mungu?”

Akasema, “Kwa sawa.”

Kisha nikasema, “Je, utakuwa mvulana mzuri baada ya Bwana kukuponya?”

Akasema, “Kwa sawa.”

²⁴ Na kila kitu nilichomwambia, “Kwa sawa.” Tukaja kugundua, alijua tu maneno mawili matatu, na moja la hayo lilikuwa, “Kwa sawa.” Kwa hiyo, ilikuwa ni sawa basi.

²⁵ Tukaenda kwenye hifadhi, huenda kuna watu hapa waliokuwa huko kwenye hifadhi ya San Carlos usiku huo, maelfu yao walikusanyika huko nje kwa ajili ya maombi. Nao Wahindi, yeye sana sana si . . . hana budi kujua analofanya, yeye hajiingizi tu kwenye chochote kile. Nilipokuwa nikizungumza, mimi, kwa namna fulani nipate kibali kwao, nami . . .

²⁶ Kama kuna mtu yeyote, wa taifa lolote, wa watu wowote ulimwenguni ninayemsikitikia, ni Mhindi. Hiyo ni kweli. Walipata maonevu mabaya, machafu kutoka kwetu. Hiyo ni kweli kabisa. Kama kuna doa lolote kwenye bendera ya Marekani, ni ya vile wanavyomtendea Mhindi. Kumnyang’anya kondoo wote, kumweka huko nje katika nchi kavu sana ulimwenguni, na kumpa dola kumi kwa mwezi za kuishi, ama chochote kile, hilo si sawa. La, bwana. Hata hivyo, nchi hii ni yake, Mungu alimpa hii, tukamnyang’anya, hiyo ni kweli kabisa.

²⁷ Na kwa hiyo, sikuzote niliwahurumia hao maskini walioishi huko nje, na sikuzote nilitaka kuomba pamoja nao. Na kwa hiyo, nilimwahidi Bwana huko Phoenix kama angemponya yule mlevi sugu na yule mwanamke mwenye kifua kikuu ya kwamba ningeenda kwenye hifadhi, ndipo wote wawili wakarudisha

hati kwamba waliponywa. Kwa hiyo basi, nikaenda kwenye ile hifadhi, na usiku huo walinisimamisha kwenye maskini mlango mdogo wa Assembly of God, kitu kama ukumbi mdogo kwenye maskini hiyo Assembly. Kulikuwako na mama mmoja, baadhi yenu ndugu wa Assembly huenda... [Ndugu mmoja anasema, "Dada Marshall."—Mh.] Dada Marshall, hivyo ndivyo huyo mama alivyoitwa, alikuwa ndiye mmishenari kule juu.

²⁸ Nami nikasimama pale na kuzungumza nao wote, nao wameketi pande zote, maelfu yao huko nje. Nao... Inapendeza kuwaona wameketi juu ya mablanketi yao na kadhalika, wakingojea ibada. Na kwa kawaida ninapofanya wito wa madhabahuni, kungekuwa na mkanyagano.

²⁹ Lakini sasa, nilisema, "Sasa, wote wanaotaka kuombewa," usingeweza kuzungumza lugha yao, nasi, katika siku hizo, hatukugawa kadi za maombi, kwa vyovyote vile, kwa hiyo nikasema, "wote wanaotaka kuombewa, na wasimame." Hakuna mtu aliyesimama. Nikawaza, "Vema, ajabu hii." Kidogo ilinishangaza. Hakuna mtu aliyesimama, vema, nikasema, nikamwambia mkalimani, nikasema, "Je, ulisema nilivyosema?"

Kasema, "Kila neno."

³⁰ Nikasema, "Naomba niliseme tena: Wote wanaonitaka niwaombe kwa ajili ya uponyaji wao, na wasimame."

³¹ Hakuna mtu aliyesimama. Kwa hiyo Dada Marshall akaja kutoka nyuma ndani pamoja na mama mmoja Mhindi. Waapache ni watu wakubwa mno, wao ni watu wakakamavu, wenye misuli. Ndipo mama mmoja akatokea, nami nilikuwa nikimwangalia dakika moja tu, nami nikasema, "Sasa, huyu mama ni mgonjwa, ana ugonjwa wa zinaa, bali si kwa sababu ya maisha machafu, ni kwa sababu hana budi kuishi jinsi anavyoishi."

Ndipo huyo mama akaniangalia kana kwamba anawazia, "Kwani ulijuaje hilo?"

³² Nami nikaomba pamoja naye, na kitambo kidogo, mtu fulani akatokea, alikuwa na ile glakoma ya macho. Ndipo aliyefuata alikuwa ni m—m—msichana mdogo, naye alikuwa ameinamisha maskini kichwa chake, na—nami nikasema, "Vema, unaweza kuangalia hukuu, kipenzi?"

"La." Bila shaka hata asingeweza kuelewa nilichokuwa nikisema.

³³ Nami nikasema, "Vema, Bwana anaweza kulifunua." Ndipo basi ikasema alishikwa na homa, ndipo akawa kiziwi katika masikio yote mawili. Naye, akiwa kiziwi, akawa bubu pia, asingeweza kuzungumza wala kusikia.

³⁴ Ndipo nikamchukua huyo msichana mdogo mikononi mwangu, na nikasema, "Bwana, tafadhali... Mimi... Sisi, hatuombi miujiza, hatuombi mambo hayo. Lakini kama

ungefanywa, ingewasaidia watu, na kama ungeufanya tu, ninataka kupata kibali kwa maskini watu hawa, waliokataliwa.”

³⁵ Ndipo nilipomwombea huyo msichana mdogo, nikamketisha chini, nikasema, “Niangalia.” Akaangalia juu namna *hiyo*. Nikasema, “Unampenda mama yako?” namna hiyo, naye akaanza kugugumiza jambo fulani. Ndipo nikajua angeweza kusikia, nikasema, “Mnaona anaweza kusikia, lakini labda atazungumza vizuri zaidi.”

³⁶ Naye mama akisimama pamoja na maskini msichana huyo, akasema, “Hmm! Anaongea vijuri sana sasa.” Kamwe nisingeweza kuelewa—nisingeweza kuelewa alichokuwa akisema.

³⁷ Halafu—halafu wa pili alikuwa ni mvulana mdogo, mwenye mkengeza. Sijawahi kamwe maishani mwangu kumwona Mungu akimkatalia mtoto mwenye mkengeza. Nakisia ni kwa nini, ni kwa sababu wakati mtoto wangu mchanga, nilipokuwa tu mvulana, nilimpoteza mke wangu na mtoto mchanga, mwajua, naye maskini msichana huyo mdogo aliteseka sana, mpaka macho yake yakawa na mkengeza, nami nusura nizimie tu, nikimwangukia. Wala kamwe nisingeweza kuvumilia kumwona mtoto mwenye mkengeza, Bwana daima hujibu maombi kwa ajili yake.

³⁸ Ndipo wakati maskini macho ya mvulana huyu mdogo wa Kihindi yakiwa na mkengeza, basi nilimchukua maskini huyu jamaa mkononi mwangu na kuomba. Ni—nilijua Mungu alikuwa amefanya hivyo, ndipo nikasema, “Kabla hata sijamgeuza huyu mvulana mdogo, kama macho yake hayajanyoka kabisa, basi mimi ni nabii wa uongo.” Nikamgeuza pale, basi nena kuhusu mstari wa maombi! Tulikuwa na mkanyagano.

³⁹ Nami nikamwuliza mkalimani. Kasema, “Walidhani yalikuwa ni mambo ya bandia hapo kwanza, lakini sasa wanaona ni ya kweli.”

⁴⁰ Kwa hiyo basi, aliye fuata alikuwa ni mama mzee Dada Marshall alikuwa akimtoa humo ndani. Na maskini, huyo bikizee, kama kuna Mhindi hapa, tafadhali msifikiri ninasema jambo hili, nikirushia kitu fulani kuhusu kuwa maskini, lakini labda maskini huyo dada alikuwa ninii sana, asingeweza kununua mikogonjo, kwa hiyo alikuwa na vifito vya ufagio vyenye, ambapo walikuwa wamekata ubao mdogo kwa msumeno na kuufunga kwa matambara.

⁴¹ Naye alikuwa ndiye anayefuata, yabisi kavu. Naye alikuwa amekakamaa sana, angechukua vijiti hivi, na kuweka kimoja namna *hii*, halafu hicho kingine, kisha apige hatua zake namna *hiyo*, halafu angevisukuma mbele, apige hatua chache fupi, ndipo alipopata...

⁴² Kuna de—desturi, wakati mwingine, ya Wahindi kusuka ngozi katika nywele zao, halafu akaniangalia, maskini macho

hayo, yanayoonekana meusi, na makunyanzi hayo makubwa, yenye kina kirefu mashavuni mwake, ninii, na machozi yakipenya chini kama vishimo vidogo kupitia mashavuni mwake. Akaniangalia namna hiyo, nikawaza, “Ee Mungu, mama wa mtu fulani. Hapana shaka mikono hiyo imeyafuta macho mengi ya watoto wadogo wanaolia, labda kamwe hajawahi kula milo mingi mizuri maishani mwake mwote.”

⁴³ Nawe huna budi kuzama ndani uwahurumie watu kama utawaombea. Na kwa hiyo, nikiwa nimesimama nikiangalia hayo, yeye aliniangalia tu, halafu akaanza kutabasamu, kamwe sikuomba wala kufanya lolote. Alishika tu mkongojo mmoja kwa mkono mmoja, mmoja kwa mwingine, kisha akanikabidhi, na kuondoka jukwaani akitembea vizuri tu kama mtu yeyote yule. Rahisi tu hivyo. Mnaona? Sasa, tu—tunajaribu kulifanya gumu.

⁴⁴ Je, ni sawa kwa jambo lingine moja tu dogo kuhusu...? Ilikuwa yapata saa tisa usiku, nilikuwa ningali nimesimama mstarini. Nami nikasema, “Nitawaombea wote,” maana ilinibidi kuondoka kesho yake. Nami nikawaona wote wakija wamelowa maji mpaka *huku* juu sana, nami nikasema, “Kwani kuna nini... Mbona—mbona wamelowa maji?”

⁴⁵ Kasema, “Vema, walikimbia kwenye hi—hifadhi nao wanawaleta wapendwa wao.” Ndipo kasema, “Hawangojei kushuka kwenda yapata maili kumi kivukoni.” Kasema, “Wanavukia mtoni moja kwa moja pamoja nao, wamewabeba mgongoni mwao, ama njia yoyote ile, kuwaleta pale.”

⁴⁶ Ndipo basi mimi... Wakija, wakisukuma kutoka upande mmoja, wakiingilia mlango wa nyuma na kutokea wa mbele, kulikuwa na m—m—mtu aliyechukua ubao na kuingamanisha vijiti viwili juu yake, naye alikuwa na jamaa mzee mwenye mvi amekingamanisha miguu na mikono yake magotini mwake hapa, na kulikuwa na Wahindi wawili wakubwa mno, wenye maungo makubwa wamembeba. Na mmoja alikuwa amesimama pale, nayo midomo yake ilikuwa samawati kabisa, na akitetemeka tu kwa baridi, amelowa maji mwili mzima.

Nami nikasema, “Unazungumza Kiingereza?”

Akasema, “*Kidogo*.”

Nami nikasema, “Hivi hudhani utashikwa na nimonia, kwa kulowa maji?” Kuona yale angesema, mwajua, kuijaribu tu imani yake.

Akasema, “Yesu Kristo amenitunza, nilimleta baba yangu.”

Nikasema, “Baba yako ana shida gani?”

“Yeye ni mgonjwa.” Alikuwa akitetemeka, alikuwa amepooza, namna *hiyo*, maskini jamaa huyo mzee amelala pale, mwajua.

Nami nikasema, “Je, yeye huzungumza Kiingereza?”

“La.”

⁴⁷ Nikasema, “Vema, mleteni hapa.” Wakampisha. Nadhani, ndugu yake alifuata, alionekana mtu mdogo zaidi wa umri amebewa, wakampisha. Nikaweka mikono yangu juu yake, nikasema, “Bwana, Bwana na akubariki.” Nikasema, “Yesu msaidie maskini mtu huyu mpendwa asiyeweza kujisaidia, heshimu imani ya mwanawe aliyemleta.” Kasema, “Vema, mpisheni.”

⁴⁸ Nami, kwa dakika moja tu, ni—nikasikia kitu kikipiga mayowe na kupiga makelele, nikaangalia pande zote, maskini yule Mhindi alikuwa amejitwika ubao begani mwake mwenyewe, akienda huku na huku akimpungia kila mtu mkono, akienda moja kwa moja . . . ? . . .

⁴⁹ Ambapo mara nyingi sisi watu wenye nyuso zilizopauka, mnaona, tunaketi tu, na, “Vema, niombe tena, ni—nitarudi nipitie mstarini, ama . . .” Loo, jamani! Wao wanaamini tu, hivyo tu, imani ya kitoto tu. Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya hilo, mnaona, kuamini tu, si jambo gumu.

⁵⁰ Huko chini katika Jiji la Meksiko mwaka jana, wakati Jemadari Medina, yule, wengi wenu ninyi ndugu, nadhani, mnamjua Jemadari Medina ni ninii, mmoja wa majemadari mashuhuri katika jeshi la Meksiko. Nilikuwa na majaliwa ya kuwa Mprotestanti wa kwanza aliyepata kualikwa kwenye Jiji la Meksiko kuwaombea wagonjwa, ama kufanya mkutano, na jeshi la Meksiko, na hiyo ilikuwa kupitia Jenerali Medina. Ndio kwanza nikutane naye hivi majuzi mkutanoni, Wafanyabiashara wa Full Gospel, nikapeana mikono naye. “Jaribu urudi tena.”

⁵¹ Tulikuwa huko siku tatu tu usiku. Nilikuwa nimeenda kwenye uwanja wa michezo ya ng’ombe, bali hatukuupata huo, kwa hiyo walikuwa na mahali pakubwa mno huko nje uwanjani, pakubwa, kitu kama uwanja mwingine mkubwa. Nao hao watu, sasa, nena kuhusu kumhitaji Kristo! Walikuja pale saa tatu asubuhi, hakuna mahali pa kuketi, wala hata sikufika mpaka saa tatu usiku. Wangeegemeana tu, kama kondoo waliosimama kondeni.

⁵² Nami ninakumbuka usiku wa pili, mvua ikinyesha, maskini hao watu wamesimama huko kwenye mvua, ninii tu, watu wa Meksiko. Na usiku uliotangulia, mwujiza mkuu ulikuwa umefanywa. Kulikuwako na mzee mmoja aliyekuja jukwaani.

⁵³ Na Meksiko, uchumi wao hauna uwiano mzuri sana. Labda, tuseme Pancho anatengeneza, yeye ni mwashi, anapata peso nane kwa siku, naye ingembidi kufanya kazi siku nne kujinunulia jozi ya viatu. Sasa, huo ndio uwiano wa uchumi huko Meksiko. Lakini hata hivyo, inawabidi kulipa senti hamsini kutoka kwa hizo wapate kuwasha mshumaa wa grisi kwenye madhabahu ya dola milioni moja. Lakini basi tunapokuja . . .

⁵⁴ Mzee huyu alikuja pale, naye alikuwa kipofu, angekuwa rika ya baba yangu, kama yeye, baba yangu, angaliishi. Wala hakuwa na viatu, maskini miguu yake imejaa sugu, na miguu ya suruali yake imechakaa, amevaa shati lililojaa mavumbi, kofia kuukuu, nayo imefungwa kwa nyuzi, na—naye alikuwa akikaribia na wa pili mstarini.

⁵⁵ Na kwa hiyo, wakamwambia, “Mwingine.” Na Ndugu, mmoja wa wainjilisti wa Assembly of God pale, Espinoza, nyote huenda mnamjua Ndugu Espinoza kutoka California, a—alikuwa mkalimani wangu, naye akamwambia ndiye aliyefuata. Ndipo akaingiza mkono mfukoni, akatoa rozari ndogo, akaanza kuikariri.

Nikasema, “Hiyo haihitajiki.”

⁵⁶ Naye akaja, nami nikamwambia. Loo, jinsi jamaa angejisikia! Mzee fukara, labda kamwe hakupata chakula kizuri maishani mwake, wala hakuwa na viatu, mimi huyo hapo nimesimama na suti nzuri na jozi nzuri ya viatu. Nikaweka mguu wangu kando ya wake, nione iwapo viatu vyangu vingemtoshia, ningempa viatu vyangu papo hapo. Nayo mabega yake yalikuwa mapana zaidi kuliko yangu, koti langu lisingemtoshia. Halafu huyo hapo katika upofu.

Nami nikamkumbatia tu huyo jamaa mzee, na kuomba, “Ee Mungu, uturehemu.”

⁵⁷ Mara, nikasikia, “Gloria a Dios!” Naye huyo hapo akikimbia huku na huku jukwaani, angeweza kuona vizuri niwezavyo ama uwezavyo wewe, akiwa tu na wakati mzuri sana.

⁵⁸ Halafu kesho yake usiku, kukiweko na jukwaa refu kama chumba hiki kilivyo hapa, lundo la makoti makukuu, na skafu, na shali urefu *huo*, zimelundikwa pale zipate kuombewa. Jinsi wangejua lilikuwa ni la nani, sijui mimi.

⁵⁹ Halafu basi, huku mvua inanyesha, hizo zikilowa maji, moja kwa moja huko nje, uwanja mkubwa mno. Ndipo Billy akaja akaniambia, akasema, “Baba, wewe . . . kuna mwanamke huko chini aliye na mtoto mchanga aliyekufa asubuhi ya leo.” Kasema, “Huwezi kumdhiti kwa vyovyote.” Kasema, “Anapanda moja kwa moja juu ya hao mabawabu, akitembea juu ya mabega yao akiwa na mtoto huyo mchanga.” Kisha kasema, “Tumemsukuma nje ya jukwaa mara tatu au nne, hatuwezi kufanya lolote, huna budi kuja huku na kumwona.”

⁶⁰ Ni wangapi wanaomjua Jack Moore, Ndugu Jack Moore kutoka Shreveport, Louisiana? Nadhani wengi wenu mnamfahamu. Vema, alikuwa pamoja nami, nami nikasema, “Ndugu Jack, nenda kule ukamwombe maskini mama huyo,” nami nikasema, “kwa ajili ya huyo mtoto mchanga.” Nikasema, “Amekufa tangu asubuhi ya leo.” Nikasema, “Hilo kwa namna fulani litamfariji.” Nikasema, “Siwezi kumleta hapa, hana kadi ya maombi.” Nami nikasema, “Isingekuwa sawa kwa watu

walio na kadi za maombi, walipata kipaumbele cha kutangulia kwenye mstari wa maombi, walisimama hapa mapema asubuhi ya leo na kuchukua kadi hizo.”

⁶¹ Na kwa hiyo, Ndugu Jack akaanza kwenda ku—kumwona huyo mama. Nami nikaangalia tu kwenye kusanyiko, ndipo nikamwona mtoto mchanga katika ono, akipiga kelele tu, akipiga makofi kwa mikono yake midogo, mtoto mchanga wa Kimeksiko. Nikageuka, nikawaza, “Vema, mimi, labda afadhali niende kule.” Nikasema, “Mleteni huku.”

⁶² Na kwa hiyo, wakafanya njia. Maskini msichana mrembo, yapata, ningesema, umri wa miaka ishirini, alikuwa na blanketi ndogo namna *hii*, na maskini mwili huo ulikuwa chini ya blanketi. Basi akapiga magoti, akaanza kupiga mayowe, “Padre,” mwajua.

⁶³ Nikasema, “Hebu—hebu simama tu, dada.” Ndipo nikamwekea mikono huyo jamaa. Nisingeweza kuzungumza Kihispaniola, basi—basi nikamwekea mikono maskini huyo mtoto mchanga, Mungu Mbinguni, ambaye Ndiye Mwandishi wa Biblia hii anajua ni kweli, nikaweka mikono juu ya maskini mtoto huyo mchanga, na muda si muda mwajua, mlio ukatokea, naye akaanza kulia, kuruka, na kupiga mayowe.

⁶⁴ Ndipo nikasema, “Sasa, usiseme lolote kuhusu hili, usichapishe hili kwenye gazeti lolote, mpaka utakapoondoka na kumwacha daktari atie sahihi taarifa ya kwamba mtoto huyo mchanga alikufa asubuhi ya leo.” Mnaona, kulikuwa na yapata... Tangu saa tatu asubuhi hiyo, mpaka yapata saa tatu na nusu, saa nne usiku huo, mtoto huyo alikuwa amekufa.

⁶⁵ Nao wakapata taarifa ya daktari wao iliyotiwa sahihi kwamba alintangaza huyo mtoto amekufa asubuhi hiyo saa tatu. Na hiyo ilikuwa saa nne, karibu saa nne usiku huo, kati ya saa tatu na nusu na saa nne. Naye huyo mtoto mchanga yu hai leo, kwa imani rahisi tu. Sikuwa na uhusiano wowote na kuponywa kwa huyo mtoto mchanga. Hakika ono lilikuja, lakini wakati ono linaponena, hakuna kitu kinachoweza kuligeuza hilo, daima ni kamilifu, daima ni kamilifu.

⁶⁶ Na katika kuwaombea wagonjwa, usiku wa leo tunapowaombea wagonjwa, Bwana anaweza kutujia na kutupa maono, na kama akifanya hivyo, kumbukeni ono haliwaponi watu, ono ni thibitisho tu kwamba Neno ni kweli.

⁶⁷ Ni wangapi wanaojua maana ya neno *nabii*? Hakika, mnajua. *Nabii* maana yake ni “mtu anayetabiri, ama kubashiri awali.” Na ni ishara ya Kiungu kutoka kwa Mungu ya kwamba mtu huyu anayenena ana tafsiri sahihi ya Neno la Kiungu, kwa sababu, “Neno la Bwana liliwajia manabii.” Naye nabii alitabiri na kufanya ishara hizo, ambazo ni thibitisho ya kwamba alikuwa na tafsiri ya Neno.

⁶⁸ Mnaona, ishara ina sauti. Musa aliambiwa, Mungu alimwambia Musa, aliposema afanye ishara kwa mkono wake, kisha afanye ishara kwa fimbo, Akasema, “Wasipoisikia sauti ya ishara ya kwanza, wataisikia sauti ya ishara ya pili.” Kila ishara ina sauti, na Sauti ya Mungu hunena nasi.

⁶⁹ Na kama Yeye akifanya hivyo, basi ninataka kila mmoja wenu ninyi watu kuamini kwa moyo wenu wote kwamba Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa kukuponya. Na sasa kumbukeni, wakati Yeye anaponena, anaponena, sio mimi.

⁷⁰ Sasa, nilichukua siku mbili usiku wa mahubiri makali sana, mazito, wala ni—nisingeomba msamaha kwa yale niliyosema, kwa sababu ni kweli, marafiki. Ni—ni—nina bidii kwa Kanisa. Na usiku wa leo, kusikia kundi hili la watu, nimeketi pamoja na wanaume zaidi katika makundi, bali kamwe sijaketi na kundi zuri zaidi la ndugu halisi wanaoamini, ambao, alinikumbatia alipokuwa akija dakika chache zilizopita, na kusema, “Tunauthamini ujumbe huo jana usiku.”

Nikasema, “Ulikuwa ni mkali sana.”

Akasema, “Lakini unatutia moyo kusonga mbele, pia.”

⁷¹ Ni—ni—nina imani na watu kama hao, naam, bwana. Naam. Tunapochukua... Kama—kama nilikuwa nikisema tu ili nionekane mwerevu, basi hilo lingekuwa ni kosa, Ni—ninapaswa kwenda madhabahuni na kujiweka sawa na Mungu. Lakini wakati ikiwa ni kweli, enyi marafiki, basi tunapaswa kujilinganisha na yale Mungu asemayo, mnaona, hiyo ni kweli; Mungu anajua.

⁷² Usiku mmoja juma hili, ninataka kuwaambia jambo fulani lililonipata yapata mwezi mmoja uliopita, nanyi mtaelewa basi kuhusu jambo fulani lililotukia. Kama lilikuwa ni ono ama silo, sijui. Niliwaelezea ndugu kwenye kiamshakinywa, nami nilitaka kuonana na wenyevit na baadhi ya wanakamati kama ni sawa kulizungumzia hapa jukwaani usiku fulani, jambo lililotukia, kama ono, kwangu mimi.

⁷³ Nami na—nawapenda watu, ninawapenda tu watu, nami ni—ninataka kuishi milele pamoja nao, nataka kuishi katika Umilele pamoja nao. Nami ni afadhali niwachochee kidogo tu sasa, kuliko kuwasikia mkisimama pale kwenye Siku hiyo kama msichana yule aliyekufa katika mji wetu hivi majuzi.

⁷⁴ Basi kulikuwa na msichana aliyekuja maskanini kule juu, yeye ni maskini msichana wa mtindo wa kale, na—na kwa hiyo, msichana huyu alimdhihaki, akamwita wa mtindo wa kale, na kila kitu. Na—naye akamwomba aende pamoja naye kwenye dansi, ndipo huyo msichana kutoka maskanini akasema, “Hatuendi kwenye dansi.”

⁷⁵ Akasema, “Huyo mchungaji wenu mwenye mawazo finyu, Bw. Branham,” akasema, “kama hakuwa mwendawazimu namna hiyo na mshupavu wa dini, mngekuwa na uhuru zaidi.”

⁷⁶ Akasema, “Sifanyi hivi kwa sababu ya imani ya Bw. Branham, ninafanya hivi kwa kushawishika kwangu mwenyewe juu ya Yesu Kristo.” Hmm! Mungu ambariki msichana huyo. Mama huyu aliyemwambia hivyo alikuwa ni mwalimu wa shule ya Jumapili.

⁷⁷ Bw. Perkins hufanya kazi ya, kwa mzishi kule mjini. Yapata miezi sita baada ya tamshi hili kutolewa, msichana huyu akawa mgonjwa akafa, hawakujua ilikuwa ni nini, ulikuwa ni ugonjwa wa zinaa. Bw. Perkins, alipokuwa akisukumia maji ya kuhifadhi maiti katika mwili wa msichana huyo, aliendelea kunusa kitu fulani, kilikuwa ni kama kinavuja. Ndipo akamfungua, naye alikuwa na matundu yaliyomla namna hiyo, kutokana na ugonjwa wa zinaa. Hiyo ni kweli. Na, nafasi kubwa ya kufanya mzaha, kusema mtu fulani ni mshupavu wa dini.

⁷⁸ Wakati alipokufa, kama ni sawa, nitawaambia huo ushuhuda, wakati msichana huyo alipokufa, alilingiza darasa lake lote la shule ya Jumapili, walipaswa wamtazame akienda Nyumbani Mbinguni, bila shaka. Lakini alikuwa wa kilimwengu sana, wa kilimwengu sana, sana. Ndipo alipokuwa tayari kufa, alifikiri ilikuwa ni sawa. Mwajua, “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.” Vema, msichana huyu, wakati alipokuwa tayari kufa. . .

⁷⁹ Mchungaji wake alivuta sigara kwenye kishikio, kishikio kirefu. Alivaa moja ya kola hizi zilizopinduliwa, hilo ni sawa kabisa, kama anataka kufanya hivyo, lakini laiti angehubiri tu Injili!

⁸⁰ Yesu, sidhani Yesu alijionyesha tofauti na mtu mwingine yeyote, alivaa kama watu wa kawaida, na akaenda miongoni mwa watu, Yeye alikuwa ni Mwanadamu miongoni mwa wanadamu. Na kwa hiyo, Yeye alikuwa ni Mfano wetu inapofikia kwenye mavazi, ama chochote kile. Sidhani inatubidi kuvaa, nafikiri maisha yetu yananena vizuri zaidi kuliko mavazi yetu yanavyofanya, ya kile tulicho. Na kwa hiyo basi, hii. . .Sio kupuza hilo hata hivyo.

⁸¹ Lakini mtu huyo alikuwa nje ukumbini, na—na kwa hiyo wakati msichana huyo alipokuwa tayari kufa, wakati mauti yalipomgusa, badala ya kuona Malaika wakija, yeye alisema, “Mungu wangu, nimepotea!”

⁸² Nao wakamwita mchungaji, naye akasema. . .akasema, “Hapa, hapa, hapa, hapa, hapa!” Kasema, “Unajua uko sawa,” kasema, “umekuwa mfuasi wa kanisa.”

⁸³ Akasema, “Ewe mdanganya watu! Wewe ndiwe chanzo chake, mimi nimeelekea kuzimuni, na wewe ndiwe uliyelisababisha!”

⁸⁴ Ndipo akamwita yule msichana ambaye alikuwa amemwambia hayo kule maskanini, maskini Bibi Humes, lakini hawakumfikisha kule kwa wakati unaofaa, msichana huyo alikufa katika hiyo...Naye—naye huyo mhudumu akasema alikuwa ameshikwa na mpagao, na akamwomba daktari aje ampe kituliza akili, lakini alikuwa ameondoka kabla daktari hajafika pale, akisema kila namna ya mambo maovu dhidi ya mhudumu huyo.

⁸⁵ Ndugu, dada, ningechukia kusimama mbele ya mmoja wa watu niliowahubiri hapo awali na kumsikia mtu akiniambia hivyo. Kama itanibidi kulifanya kali sana wakati mwingine, A—afadhali niwe hivyo na niwe mwema, na safi, na mnyofu mbele za Mungu wakati utakapowadia.

Sasa, kabla hatujalifungua Neno Lake, hebu na tuombe, tunapoinamisha vichwa vyetu.

⁸⁶ Baba Mtakatifu na Mwenye Neema sana, tunakikaribia kiti Chako cha Kiungu cha haki usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu, tukisihi Damu Yake ije juu ya nafsi zetu tusije tukasimama katika hukumu. Lakini, hata hivyo, bila hiyo Damu iliyomwagika, sote tungehukumiwa, wala kusingekuwa na njia kwetu kamwe kukukaribia Wewe.

⁸⁷ Lakini tuna jambo hili lililobarikiwa kutoka Kwake: “Kwamba mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, Yeye atalifanya.” Basi Baba, tunaomba usiku wa leo ya kwamba utatusamehe makosa yetu, lolote ambalo tumefanya, ama kusema, ama tulilodhania kwamba lilikuwa ni kosa, tusamehe hilo.

⁸⁸ Kama ni mapenzi Yako ya Kiungu, tunapaswa kuwaombea watoto Wako wagonjwa, wanaoteseka katika muda mfupi tu. Tunakaribia somo fulani katika dakika chache kujenga jukwaa, tuseme, kusudi imani ya watu ikae juu ya msingi huu wa Neno, Neno la Mungu la Milele. Je, utatupatia, Bwana, muktadha wa somo ambalo nimechagua kwa ajili ya alasiri ya leo? Jalia Roho Mtakatifu alichukue Neno, na kuliweka katika kila moyo sawasawa na mahitaji yetu. Unajua mahitaji yetu, Bwana, nasi tunaomba ya kwamba utapanda mbegu ya Injili mioyoni mwetu, mpaka itakapokua ikawa miti mikubwa ya wokovu, na faraja, na afya kwa kila mmoja.

⁸⁹ Nazo leso hizi zilizowekwa hapa, Bwana Mungu, ninaweka mikono yangu juu yazo katika ukumbusho wa Mtakatifu Paulo, aliyefanya agizo hili, tukiamini ya kwamba alilipata katika Biblia, ambapo Elisha alichukua ile fimbo na kumwambia Gehazi, “Nenda ukaiweke juu ya huyo mtoto mchanga.” Kwa kuwa alijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilibarikiwa, naye alijua ya kwamba fimbo hiyo ingeninii... ilikuwa imebarikiwa, kwa sababu wakati Roho Mtakatifu alikuwa juu yake, mikono yake ilikuwa juu ya ile fimbo, na halafu kumfanya mwanamke

huyo kuliadini. Ninaadini hapo ndipo Mtakatifu Paulo hapana shaka aliyapata hayo Maandiko.

⁹⁰ Sasa, lesa hizi zinawakilisha, hapana shaka, watoto wagonjwa, baba wagonjwa, mama, wapendwa, nyumba za mapumziko. Baba kipofu ameketi mahali fulani chumbani akigongesha fimbo nyeupe sakafuni, akitaka kuona nuru ya jua tena, anataka kuona miti, yale maji mazuri, ya samawati, lakini adui amefunika macho yake kwa watoto wa jicho; mama amelala pale, mgonjwa; mtoto mchanga mwenye homa, akingojea kurudi kwa lesa hizi. Ee Bwana, nisikie, Bwana, naomba.

⁹¹ Imelandikwa, wakati mmoja, ya kwamba wana wa Israeli walikuwa wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, nayo Bahari ya Shamu ikaingia njiani. Na imesemwa na mwandishi mmoja, ya kwamba Mungu aliangalia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, nayo Bahari ya Shamu ikaogopa, ikarudi nyuma, nao Israeli wakasonga mbele kwenda kwenye nchi ya ahadi.

⁹² Ee Baba wa Kiungu, naomba usiangalie tu kupitia kwenye Nguzo ya Moto, bali kupitia Damu ya Yesu. Na wakati ishara hizi ndogo zinapopelekwa kando ya vitanda vya wagonjwa na wanaoteseke, ama popote walipo, naomba uangalie kupitia Damu ya Bwana Yesu, tunajua ya kwamba alikufa pale Kalvari na alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa, jalia adui aogope, aondoke, na jalia watu wagonjwa waingie kwenye nchi hiyo nzuri ya afya, ambayo imeandikwa katika Maandiko, “Juu ya yote nataka mfanikiwe katika afya zenu.”

⁹³ Tujalie, Bwana, jalia kila ugonjwa uwaondokee watu, kwa kuwa tunawatuma, katika Jina la Yesu Kristo, kwa kusudi hilo, wakati kanisa hili kuu hapa usiku wa leo linapoomba pamoja nami. Amina.

⁹⁴ Sasa, mnaweza kuja na kuzipokea mara tu ibada itakapokwisha. Na kama unataka moja na huna moja hapa, niandikie tu, kila kitu ni bure, hatuna kitu tunacholipisha. Niandikie tu wakati wowote huko Jeffersonville, Indiana, tutakutumia moja. Kama huna haja nayo, iweke katika Biblia yako katika Matendo mlango wa 19, ndipo ugonjwa ukitokea nyumbani nawe unaadini, sasa, chukua lesa hiyo ndogo na kuweka juu yao, itatimia, tunaadini ya kwamba Mungu ataponya. Tungalikuwa na wakati, tungetoa shuhuda nyingi za jambo hilo, bali sina wakati sasa.

⁹⁵ Hebu na tufungue Biblia zetu, ninyi mnaoyaandika Maandiko, kwenye Luka Mtakatifu mlango wa 18, kifungu cha 37 na 38, kwa ajili ya fungu dogo tu.

⁹⁶ Na sasa wakati mkifungua, huenda labda kesho usiku na kuendelea, hatujui, jinsi tu Roho Mtakatifu atakavyoongoza, tunaadini ya kwamba labda tutakuwa tukiwaombea wagonjwa

muda uliosalia wa juma hili kila usiku, tukichukua wachache kila usiku, na kile tuwezacho, na mradi wagonjwa waje na wanataka kadi za maombi wapate kuombewa.

⁹⁷ Sababu ya sisi kuwapa kadi za maombi ni kuwapanga mstarini. Mnaona? Ungesema, labda tuseme kuna watu elfu moja hapa usiku wa leo, labda mia tano kati yao wanataka kuombewa, hatuwezi kuwaleta wote hapa mara moja, tunajua hilo. Na kwa ajili ya . . . Katika mstari wa upambanuzi, tunaweza tu kuleta wachache sana, sana, sana, maana karibu inakuua. Ni wangapi wanaolewa jambo hilo, Kimaandiko? Hakika, mnalielewa. Mnaona? Na kwa hiyo, halafu hatuwezi kuleta wengi kupita kiasi, lakini usiku baada ya usiku, tutajaribu kuwaleta tu wale tuwezao.

Vema:

Wakamwambia, ya kwamba Yesu Mnazareti anapita.

Akapaza sauti akisema, Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.

⁹⁸ Ilikuwa asubuhi yenye baridi sana, alikuwa amechoka, alikuwa macho usiku kucha, hapana shaka aliota usiku kucha kwamba angeweza kuona, ndipo akachelewa kuamka. Na katika siku hizo, kulikuwa na ombaomba wengi, waliketi kando ya barabara, huku watu wakiingia, wafanyabiashara wakienda kazini mwao, labda walikuwa na sadaka za kuwapa. Basi ombaomba wa kwanza aliyekutana naye, alitoa sadaka zake, na hiyo ilitosha kwa siku hiyo, hakuwa na kitu kingine angaliweza kutoa. Kwa hiyo wengi wao walikuwa na vibanda kama, ama mahali ambapo waliketi na kungojea mtu fulani apite na kuwapa sadaka. Na kama waliikosa, vema, basi walikaa siku nzima bila.

⁹⁹ Mara nyingi walikuwa na vitu vidogo vya kutoa, vitu vidogo kama mazingaombwe. Nilikuwa India hivi majuzi, nao kila mmoja wao ana nyo—nyoka swila, ama tumbili mdogo, ama—ama *kitu kingine* kuvutia usikivu wa watalii.

¹⁰⁰ Hii hapana shaka ilikuwa asubuhi yenye baridi, yenye mzizimo, ilikuwa ni majira ya kuchipua, karibu na Pasaka. Naye alikuwa amevaa matambara, tena amechelewa, napo mahali pake palikuwa ni kuketi kwenye lango la Yeriko, jina lake lilikuwa Bartimayo. Nanyi . . . Tunaambiwa ya kwamba alikuwa ameo, alikuwa na msichana mdogo. Lakini kwa kuwa alikuwa macho usiku kucha, hakupata usingizi mwingi, alichelewa kuamka, naye akakosa wakati wa—wake wa kuomba msaada. Wafanyabiashara wengi wa nje walioishi nje ya mji walikuwa tayari wameingia, ilikuwa inaelekea mchana.

¹⁰¹ Kwa hiyo, ninaweza kuona mandhari yetu usiku wa leo inapofunguliwa upande wa kaskazini mwa lango lililoelekea—juu kuelekea Yerusalemu, lango la kaskazini la Yeriko. Mengi ya yale mawe ya kale yalikuwa yangali yamewekwa pale ambayo yaliporomoka wakati watu walipopaza sauti, naye

Yoshua na makuhani wakapiga tarumbeta, na kuta za Yeriko zikaporomoka.

¹⁰² Hebu tuwazie Bartimayo sasa ameketi kwenye moja la yale mawe, karibu na mahali ambapo ile barabara kuu ya mango ingali imesimama kama ilivyokuwa katika siku za kale, inateremka chini, ikishuka kuelekea Yordani. Ndipo alipokuwa ameketi pale, hapana shaka alikuwa akiwazia, “Sasa, labda itanibidi kukaa bila chakula, familia yangu usiku wa leo, kwa kuwa nilichelewa sana, nisingeweza kuingia. Wafanyabiashara wote wamepita, nami sitapata chochote leo. Lakini nisingeweza kujizuia, nilikuwa nimechoka sana na kudhoofika asubuhi ya leo nilipofika hapa.”

¹⁰³ Naye akaketi chini, hebu tuamini ya kwamba alianza kuwazia, “Loo, laiti ningalikuwa tu na . . . ndoto hiyo ingalikuwa ni uhalisia, kwamba ningeweza kuona tena! Nimekuwa kipofu sasa kwa miaka mingi,” angesema, “na laiti ningaliweza kuona kama nilivyokuwa nikifanya!”

¹⁰⁴ Ndipo akili yake ikaanza kurudi nyuma wakati alipokuwa mvulana mdogo, alizoea kucheza huko nje kwenye majira ya kuchipua, ambayo yangukuwa tu, loo, siku chache baadaye. Na jinsi ambavyo kwenye vilima vya kingo za Yordani, maua madogo ya manjano yanachanua huku na huku, na maua madogo ya samawati, na ni mandhari nzuri jinsi gani. Na jinsi ambavyo alikuwa akiwazia alipokuwa mvulana mdogo, jinsi ambavyo angetangatanga juu chini ya kilima hicho, na kucheza na kurukaruka na hao wavulana wengine wadogo.

¹⁰⁵ Halafu basi, anakumbuka, ya kwamba baadaye mama yake mpendwa, Myahudi, angemwita ale chakula chake cha adhuhuri, akiisha kula chakula chake cha kutwa, angempeleka nje barazani, naye angemlaza pajani mwake, na kuzipapasa maskini nywele zake kutoka machoni mwake. Naye angemwangalia, naye angeona jinsi alivyokuwa mrembo, na jinsi angesema, “Bartimayo, macho yako madogo ni ya samawati kama anga juu.”

¹⁰⁶ Loo, angewazia, “Laiti ningaliweza kuishia siku hizo mara nyingine tena, wakati ningeweza kuyaona hayo maua, na kuwafukuza nyuki kote, na kusikia ndege wa kupendeza na kuwaona, na kumwona mama yangu mpendwa, lakini ole, uzee ulimvamia, naye akapata makunyanzi na hatimaye akafa, nasi tulimzika miaka mingi iliyopita. Nami hapa ni mzee, na maskini, na fukara, nimeketi hapa nikiombaomba, kipofu.”

¹⁰⁷ Naye alizoea kuwazia jinsi alivyofurahia hadithi ndogo za Biblia ambazo angemsimulia kabla hajaenda kulala, wakati hatimaye angemvuta kifuani mwake na kumpembeza alale. Basi moja ya hadithi alizopenda, ilikuwa ni hadithi ambayo nilikuwa nikirejea tu muda mfupi uliopita, ya yule mvulana mdogo ambaye Elisha alimfufua katika wafu.

108 Jinsi mama yake alivyo zoea kumnukulia hadithi hiyo, na kusema, “Bartimayo, kulikuwa na mwanamke mashuhuri, alikuwa Mshunami, naye aliishi huko Shunemu. Naye alimwamini mtumishi wa Mungu aliyeitwa Elisha, yule nabii mkuu, mwenye nguvu.

109 “Naye alipitia nyumbani kwake mara kwa mara, basi siku moja, akamwambia mumewe, ‘Tunaona kwamba mtu huyu anayepitia njia hii ni mtu mtakatifu, yeye ni mtu mashuhuri, kwa sababu Mungu hufanya ishara kuu na maajabu kupitia kwake. Kwa hiyo nakuomba, hebu na tumpe fadhila kwa kujijengea kando ya nyumba yetu, kumjengea, hasa, chumba kidogo apate kusimama na kupumzika.’”

110 Sasa ninaweza kumwazia akimwambia Bartimayo, “Unaona, Bartimayo, tunapaswa kuwatendea watu wote mema, hatupaswi kuwa waovu kwa mtu yeyote, na, hasa, tunapaswa kuiheshimu na kuithamini nyumba ya Mungu. Kwa hiyo mwanamke huyu, alikuwa na hakika ya kwamba mtu huyu aliyemtembelea alikuwa ni nabii mkuu mwenye nguvu, wa Bwana.

111 “Na kwa hiyo, mumewe akakubaliana nalo. Ndipo Elisha na Gehazi, mtumishi wake, walipopitia tena, kulikuwa na chumba kidogo kizuri, kilichojengwa karibu na ukuta, mtungi mdogo ukiwa na maji ndani yake, na kitanda kidogo, na kibao cha kuwekea mguu, na mahali pake pa kupumzikia. Alikuwa akienda zake pangoni juu ya Mlima Karmeli, ambapo alienda kufunga na kuomba katika siku fulani, kama vile miandamo ya mwezi na sikukuu, kabla nabii hajanena mitaani.

112 “Basi Elisha alipoingia na kuona haya yote ambayo mwanamke huyu mwema alikuwa amefanya, mbona, alimtuma Gehazi, na kusema, ‘Nenda kamwulize tumtendee nini. Mimi ni rafiki msiri wa amiri mkuu wa jeshi, nami pia nitazungumza na mfalme. Naweza kuzungumza kwa niaba yake?’

113 “Basi Elisha alipomwuliza hili, mbona, yeye alisema, ‘La, ninakaa pamoja na watu wangu.’ Na loo, alikuwa mwanamke tajiri, hawakuwa na haja ya kitu, walikuwa... alikuwa amefanya hivyo kwa fadhili ya moyo wake.”

114 Na hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya jambo lolote unapolifanya kwa ajili ya Mungu, lifanye kwa fadhili ya moyo wako. Unapotoa chochote, kitoe kutoka moyoni mwako, kama huwezi kufanya hivyo, basi usilifanye, maana zawadi yako haitaheshimiwa kwa Mungu. Basi lifanye tu kwa fadhili ya moyo wako.

115 “Vema, basi huyo mtumishi aliporudi na kumwambia nabii, ‘Vema, hahitaji chochote, kila kitu kiko shwari kwake. Lakini nitakwambia jambo moja, anazeeka kidogo, na mumewe ni mzee, nao hawana watoto wowote.’

¹¹⁶ “Hapana shaka ila kwamba nabii aliona ono, kwa sababu hakuna nabii, ama mtu mwingine yeyote, aliyepata kumfanyia Bwana lolote, kwa Bwana namna hiyo, isipokuwa iwe ni kwa ono.” Sasa kumbukeni, hiyo ni kweli, tafuta mahali popote katika Maandiko ama popote pale, daima kwanza kabisa, Mungu huwaambia. Mungu... Mtu hawezi kufanya lolote kwa kubahatisha, yeye ni mtumishi wa Mungu.

¹¹⁷ Hata Yesu Kristo alisema, “Sifanyi neno Mwenyewe, ila lile nimwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile,” Yohana Mtakatifu 5:19. Na kama Mwana wa Mungu hangeweza kufanya lolote bila Baba kumwonyesha Yeye kwanza, si zaidi sana sisi bila Mungu kutuonyesha kwanza? Kwa hiyo, tunakimbilia mambo kwa ujasiri wakati mwingine bila kujua tunachofanya. Lakini wakati Mungu anapotoa ono, na kunena, na kuonyesha yale hasa atakayofanya, ni mchezo wa kuigiza tu kuucheza, hivyo tu, kwa sababu Mungu atalifanya, Yeye tayari amesema hivyo, kwa hiyo hilo linalishughulikia.

¹¹⁸ “Sasa, kwa hiyo akasema, ‘Nenda kamwite huyo Mshunami.’ Naye akasimama mlangoni, naye akasema, ‘Panapo wakati huu mwakani, utamkumbatia mtoto.’

¹¹⁹ “Sasa, yeye akasema, ‘Mimi ni mzee.’ Lakini maneno ya Elisha yalitimia kama tu alivyosema, kwa kuwa katika muda fulani wa miezi, alimkumbatia mtoto mzuri, mvulana.”

Nami ninaweza kuona maskini macho ya Bartimayo, yakisema, “Je, alimpenda, Mama, kama unavyonipenda mimi?”

¹²⁰ “Naam, kama tu ninavyokupenda. Alikuwa ni mtoto mvulana, mwenye sura nzuri, aliwazia ni mwenye sura nzuri kuliko wote ulimwenguni, kama ninavyokuwazia, kama vile akina mama wote wanavyowawazia watoto wao wachanga.

¹²¹ “Basi—basi siku moja, wakati mvulana huyu mdogo alipokuwa na umri wa yapata miaka kumi ama kumi na miwili, alikuwa huko nje pamoja na baba yake kondeni, maana baba yake alikuwa ni tajiri, mavuno yalikuwa yanaendelea, kwa hiyo alikuwa huko nje kondeni pamoja na baba yake. Nami nadhani maskini mvulana huyo hapana shaka aliugua kwa shambulio la jua kali, akaanza kulia, ‘Kichwa changu, kichwa changu!’ Ilikuwa yapata majira ya adhuhuri.

¹²² “Ndipo mmoja wa watumishi akamwingiza ndani maskini mvulana huyo, ndipo akaketi pajani mwa mama yake hata yapata adhuhuri, basi maskini mvulana huyo akawa mgonjwa zaidi, na zaidi, na zaidi, hata baada ya kitambo kidogo, maskini mvulana huyo akafa.”

¹²³ Ninawatakeni mwangalie, ambapo wakati Mungu anapoanza kumshughulikia mtu, wanafanya mambo wakati mwingine ambayo hata hawatambui yale wanayofanya. “Alimchukua maskini mvulana huyo, akamlaza katika kitanda cha nabii.” Ni mahali pa jinsi gani pa kumlaza! Penyewe

hasa. “Akamlaza juu ya kitanda cha nabii mahali alipokuwa amejenga chumba hiki kidogo, naye alikuwa amemchukua na kumlaza huyo mvulana mdogo kwenye kitanda cha nabii, naye akamwambia huyo mtumishi, ‘Tandika maskini nyumbu usonge mbele. Usimpunguzie mwendo, nisipokwambia.’

124 “Mumewe akasema, ‘Usipande kwenda kwenye Mlima Karmeli, si mwandamo wa mwezi wala Sabato, nabii hatakuwako.’

125 “Lakini moyo huo wa mama kwa ajili ya mtoto wake mchanga, alikuwa—alikuwa katika dhiki, naye alijua kama angepata kumfikia huyo nabii, kwamba angejua ni kwa nini Mungu alimchukua mtoto wake mchanga. Kama Mungu angeweza kumwambia huyo nabii yeye atampata mtoto, naye akampata, hakika, Mungu angeweza kusema ni kwa nini alimchukua huyo mtoto mchanga. Akasema, ‘Hatujambo. Endelea.’

126 “Ndipo huyo mtumishi akaenda mpaka Mlima Karmeli, naye Elisha alikuwapo. Akasimama nje kwenye mlango wa pango, akaangalia nje, naye akasema, ‘Huyu hapa yule Mshunami anakuja.’ Kisha kasema, ‘Ana wasiwasi, lakini Mungu amenificha, kamwe hajaniambia kile yeye. . . shida yake ni nini.’”

127 Unaona, Mungu hawaambii watumishi Wake kila kitu afanyacho, Yeye huwajulisha tu kile anachotaka wajue. Mnaona? Ni juu ya Mungu. Kulikuwako na mtu huyu mashuhuri, bali hakujua shida yake ilikuwa ni nini.

128 “Na kwa hiyo, akamwambia Gehazi, ‘Kimbia uende ukamlaki, ukaseme, “Hujambo?”’

129 “Naye akasema, ‘Hujambo? Mume wako hajambo? Mwanao hajambo?’”

130 Mwangalie mwanamke huyo: “‘Hatujambo.’” Amina! Ninapenda hilo. Kwa nini? Mtoto wake mchanga amelala maiti, mumewe akikunja mikono yake na kupiga mayowe, akitembea huku na huku uani, lakini, “Hatujambo.” Ninapenda hilo.

131 Kusudi lake lilikuwa ni kwenda mbele ya nabii huyu aliyekuwa na upako wa Bwana juu yake, naye alijua ya kwamba nabii huyo angejua la kufanya, la kumwambia. Alijua angekuwa na BWANA ASEMA HIVI kwa ajili yake, na kwa hiyo, “Hatujambo.” Kama Mungu alimchukua huyo mtoto mchanga, vema, mradi tu ulikuwa ni mpango wa Mungu. “Mungu alitoa, Mungu ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe.” Mnaona? Lakini alitaka kujua ni kwa nini. Je, alikuwa amefanya jambo fulani, ama ni shida gani?

132 “Basi alipokimbia mpaka miguuni pa Elisha na kuanguka miguuni pake, na kwa hiyo Gehazi akawazia huo kidogo ulikuwa ni utovu wa uadilifu kwa mwanamke kuanguka miguuni pa

bwana wake, kwa hiyo akamnyanyua juu. Na kwa hiyo, ndipo akaanza kumfunulia kuhusu huyo mtoto aliyekufa.

¹³³ “Sasa, akamwambia Gehazi, ‘Chukua fimbo yangu, uende mbele, na kuiweka hii juu ya huyo mtoto mchanga, na mtu yeyote akinena nawe, usiwazungumzie, mtu akikusalimu,’” (Hiyo ni “U hali gani?”) “‘usiseme neno, weka tu nia yako katika kuipeleka fimbo hii kwa huyo mtoto mchanga na uanze kwenda.’”

¹³⁴ Ninapenda hilo. Hatuna wakati wa kujipumbaza, Ujumbe ni wa dharura, watu wanakufa, hebu tusonge mbele.

¹³⁵ “Ndipo akaichukua ile fimbo akaondoka.”

¹³⁶ Sasa, ninaamini kama huyo mwanamke angaliamini ya kwamba hiyo ingefanya kazi, ingeifanya, bali imani yake haikuwa katika ile fimbo, ilikuwa katika nabii, “Kwa hiyo akasema, ‘Kama Bwana, Mungu wako, aishivyo wala hafi kamwe, na nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha, nitakaa papa hapa.’”

¹³⁷ Loo, napenda hilo. Lishikilie. Unapomshikilia Mungu kwa ajili ya jambo fulani, usiachilie. Hiyo ni kweli. Ukimchukua Yesu kuwa Mponyaji wako, usiache ibilisi yeyote, kitu chochote kile kikuondoshe kwake, shikilia, “Nitadumu nalo, nidumu papo hapo.”

¹³⁸ “‘Kama Bwana, Mungu wako, aishivyo na nafsi yako haifi, sitakuacha mpaka nitakapopata habari kuhusu huyo mtoto.’”

¹³⁹ Vema, Elisha asingeweza kumwondosha, kwa hiyo hivyo ndivyo unavyotaka kuwa pamoja na Yesu. Unataka tu kuingia mikononi Mwake, ukae tu hapo, ulie mchana na usiku, hiyo ndiyo njia. Naam, bwana. Kamwe usiachilie, usirudi nyuma hata kidogo, kama unaamini, kaa hapo. Kuna rehema katika Bwana. Kaa nayo.

¹⁴⁰ Kwa hiyo, nafikiri hiyo ndiyo sababu Mariamu, ama, ilikuwa ni Martha, aliyetoka kwenda kumlaki Yesu, alijua, alikuwa amesoma hadithi hiyo ya mtoto Mshunami, alijua kama Mungu alikuwa ndani ya nabii, hakika Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe. Naye alijua ya kwamba angepata haja yake, kama angeenda kwa njia sahihi. Hilo ndilo jambo linalofuata, Watu wanamwendea Mungu kwa njia mbaya, huna budi kuja kwa njia sahihi.

¹⁴¹ Si muda mrefu uliopita, nilipata heshima ya kumwombea mfalme fulani. Walitoa sijafu kutoka miguuni mwa suruali yangu, wakaniambia kamwe nisirudi nyuma, nisimpe kisogo, baada ya maombi na kadhalika, kumpa kisogo. Kamwe usimpe kisogo mfalme, hilo ni jambo zuri sana, kamwe usimpe kisogo Mfalme wa wafalme basi. Mnaona? Na ni njia ya kumwendea, njia fulani ya kumwendea.

¹⁴² Mahakamani, kuna hakimu kizimbani, na kama unajua jambo fulani huko nyuma, useme, “Hei, ngoja kidogo, Hakimu,

nataka kuzungumza nawe kidogo,” utakemewa. Kuna njia ya kumwendea hakimu huyo, nawe huna budi kuitumia hiyo.

¹⁴³ Na kuna njia unayopaswa kumkaribia Mungu. Kama ukiifikia karama ya Mungu, huna budi kuja kwa mtazamo mzuri, huna budi kuja kwa njia sahihi, la sivyo hutapokea chochote utakapokuja.

¹⁴⁴ Na hivyo ndivyo huyu Martha alivyofanya wakati Yesu alipokuja, alikuja kwa njia nzuri; huyu mwanamke Mshunami, alikuja kwa njia nzuri, akiwa na moyo uliolemewa, akimtamani Mungu, naye akashikilia.

¹⁴⁵ “Ndipo Elisha akasema, ‘Vema, nitaninii tu...’ akakaza viuno vyake, naye akamfuata.

¹⁴⁶ “Alikutana na Gehazi alipofika huko akirudi, kasema, ‘Niliweka fimbo juu ya huyo mtoto, wala hakukuwa na uhai ndani yake.’”

¹⁴⁷ Na bila shaka hamna, huyo mwanamke hakuamini hilo, kama angaliamini, lingetukia. Lakini alimtaka nabii, hakujua habari za hiyo fimbo, Elisha alikuwa na imani kwayo, lakini huyo mwanamke alikuwa na imani katika nabii.

¹⁴⁸ “Kwa hiyo wakati Elisha alipoingia chumbani,” ninawatakeni mwone, hakuna maombi, “Elisha alienda kule, nena kuhusu hali fulani! Kulikuwako na watu uani, wote wakiomboleza na kupiga makelele, naye baba amechanganyikiwa kabisa, na kila mtu akipiga mayowe. Naye maskini huyo mtoto mchanga amelazwa kitandani pa nabii, alikuwa amekufa tangu siku hiyo adhuhuri.

¹⁴⁹ “Ndipo Elisha akaingia, akatembea huku na huku,” Biblia ilisema huku na huku chumbani. Alikuwa akifanya nini? Akingojea upako. Amina. Akitembea huku na huko, loo, jamani, akingojea tu upako. “Baada ya kitambo kidogo, upako wa Roho Mtakatifu ukamjia, akaanguka kumkingama huyo mtoto mchanga, akaweka midomo yake kwenye midomo yake, pua yake kwenye pua yake, paji la uso wake kwenye paji la uso wake, kisha akalala pale. Akamhisi, akapata joto, akarudi, akatembea tena.” Loo, jamani! Ninapenda hilo.

¹⁵⁰ “Akitembea huku na huko, mpaka akahisi upako juu yake tena. Wakati upako ulipomjia tena, akaanguka kumkingama mtoto huyo mchanga tena, midomo yake kwenye midomo yake, pua yake kwenye pua yake, na muda si muda mwajua, mtoto huyo akapiga chafya mara saba kisha akafufuka.” Amina.

¹⁵¹ Loo, jinsi maskini Bartimayo alivyoipenda hadithi hiyo! Ninaipenda, pia. “Loo,” akawaza, “unajua nini? Nabii yule yule mkuu, Eliya, naye alipopaa juu, akarudisha sehemu maradufu ya roho yake juu ya Elisha, naye Elisha alikuwa ni nabii mkuu.”

¹⁵² Halafu yapata tu wakati huo, ilitokea aliwazia, “Si miaka mingi iliyopita, ambapo Eliya na Elisha walitembea kwenye

barabara ii hii ambapo nimeketi kando yake, wameshikana mikono, wakishuka kwenda Yordani kuufungua, wavuke.” Amina. Loo, jamani!

¹⁵³ Loo, upepo ukavuma naye akavuta maskini koti lake kuukuu juu kidogo, mwajua, kidogo jua lilikuwa likienda upande ule mwingine wa ukuta. Angewazia, “Si zaidi ya miaka mia chache iliyopita, Eliya na Elisha walitembea moja kwa moja kwenye maskini mawe yaya haya hapa huku wameshikana mikono, wakishuka chini. Ndipo Eliya akachukua vazi hilo na kuupiga Yordani, akasema... nao Yordani ukafunguka, Elisha akalitwaa, kisha akarudi na kuupiga Yordani, na kurudi nalo.”

¹⁵⁴ Loo, ninaweza kumsikia Bartimayo sasa, akipiga mayowe moyoni mwake na kusema, “Loo, laiti ningalikuwa tu nimeketi hapa wakati huo! Kama ningalikuwa nimeketi hapa wakati huo, ningalikimbia mtaani, na kusema, ‘Loo, manabii wakuu, watakatifu wa Mungu, niombeeni, kwamba Bwana Mungu atanifungua macho.’ Nao wangeluweka mikono yao juu yangu, nami, ndoto yangu jana usiku ya kuona tena ingekuwa ni ya kweli, ningepata kuona. Lakini ole, kuhani wangu ananiambia hekaluni kwamba siku za miujiza zimepita.”

¹⁵⁵ Loo, ilikuwa ni lini “Siku za miujiza zimepita”? Siku ya miujiza itakapopita, siku ya Mungu imepita, kwa kuwa Mungu ni miujiza. Bila shaka, siku za miujiza hazitapita kamwe, hazijawahi kupita wala hazitapita kamwe.

¹⁵⁶ “Lakini walisema ya kwamba si—siku za miujiza zimepita.”

¹⁵⁷ Yapata wakati huo, anasikia m—mlio mdogo ukishuka mtaani. Akasikiliza. “Lazima iwe ni... Ni maskini nyumbu, kuna mtu ametangulia mbio amevaa makubadhi, hapana shaka ni tajiri anayekuja.” Asingeweza kuona, bali angeweza kusikia. “Hapana shaka ni tajiri, kwa sababu amepanda nyumbu.”

¹⁵⁸ Kwa hiyo akainuka kutoka kwenye mwamba wake, akasema, “Nisaidieni! Mimi ni... Jina langu ni Bartimayo, mimi ni kipofu. Nina msichana mdogo nyumbani, mke. Tafadhalini, mwaweza kunipa sadaka? Ni—ni—nimefika hapa nimechelewa sana asubuhi ya leo.”

Ndipo yule mtumishi akasimama, na kusema, “Bwana?”

¹⁵⁹ Na ilitokea kwamba, yule jamaa pale alisema, “Sikiliza, simile ewe ombaomba, mwombaji. Mimi ni kuhani, niko njiani nikishuka kuja hapa kukutana na shirika la wahudumu. Kuna nabii mlokole nchini, anadai kuona maono, na kadhalika, na kuwaponya wagonjwa, na kadhalika, yeye ni nabii mlokole kutoka Galilaya. Nitakutana na shirika la wahudumu tukahakikishe ya kwamba hakuna ulokole kama huo utakaopata kuanza hapa Yeriko. Simile! Naenda zangu.” Hmm! “Mimi ni mtumishi wa Bwana,” (Akiwa na mtazamo kama huo!) “njiani.”

¹⁶⁰ Bartimayo akashika njia akalifikia jiwe lake tena, lakini, mwajua, jua lilikuwa limezunguka kidogo upande wa pili, na—na kwa namna fulani kukawa na kivuli pale, kwa hiyo a—akatoka nje kwenye jua tena, akajitafutia jiwe lingine na kuketi chini, akavuta vazi lake juu tena.

¹⁶¹ Akawazia, “Loo, hilo si lilikuwa ni jambo zuri kukumbuka nilipokuwa mvulana mdogo, wakati mama alipokuwa...? Loo, naam, ninakumbuka tena, aliniambia jinsi Yehova mkuu alivyowaongoza wana wa Israeli, watu wangu, wakaingia kwenye nchi hii ya ahadi, juu ya zile hadithi kuu alizosimulia jinsi Yehova alivyonyesha mikate kutoka Mbinguni na kuwalisha, jinsi alivyosababisha upepo mkuu kuwaleta kware, jinsi alivyotoa maji kutoka katika Mwamba. Loo, imekuwaje kwa huyo Yehova mkuu?”

¹⁶² “Lakini kasisi ananiambia ya kwamba siku za miujiza zimepita, kwa hiyo hakuna kitu ninachoweza kufanya juu yake. Loo, laiti ningaliishi katika siku hiyo! Laiti ningaliishi katika siku ambapo Yehova alikuwa hai kweli, na hapa duniani pamoja na watu Wake! Lakini wananiambia hayo yote yamekwisha, kwa hiyo mimi, hakuna kitu ninachoweza kufanya juu yake.”

¹⁶³ Basi alipokuwa ameketi pale, akaanza kuwazia, “Naam, nami ninamkumbuka yule shujaa mkuu, Yoshua, jinsi mama yangu alivyozoea kusema, ‘Mpenzi, *kule* ng’ambo tu, kwenye kivuko kimoja tu pale chini ya mji, Yoshua, yule shujaa mkuu mwenye nguvu aliyepachukua mahali pa Musa. . .”

¹⁶⁴ Mfano wa Roho Mtakatifu sasa, akichukua...Mnaona, Musa hakuwaingiza hao wana katika nchi ya ahadi, yeye alikuwa ndiye mtoa sheria, bali hakuwaingiza hao wana katika nchi ya ahadi, Yoshua aliwavusha. Mnaona? Naye Roho Mtakatifu Ndiye anayewavusha sasa. Kristo alifanya njia na mipango, na alikuwa ndiye Mtoa sheria, na kadhalika, bali Roho Mtakatifu hulipeleka Kanisa kwenye nchi ya ahadi, kule Kunyakuliwa, akilitwaa juu, Roho Mtakatifu katika Kunyakuliwa.

¹⁶⁵ “Na jinsi ambavyo Yoshua, yule shujaa mkuu, alivyosimama ukingoni kule baada ya kumwona Mungu akitenda kazi pamoja na Musa, naye akasimama pale, na hapo ilikuwa katika mwezi wa Aprili,” mama yake alimwambia, “na maji yote ya theluji huko Uyahudi milimani yalikuwa yakiyeyuka, nao Yordani ulikuwa umefurika kote kote kwenye nyanda hapa. Lakini yule Yoshua mkuu alisimama upande wa pili, naye akamwona Mungu, Naye akamwambia awakusanye watu pamoja, na kuwafanya wajitakase, kujiweka tayari, kwa sababu alikuwa anataka kuifungua Yordani. Na jinsi ambavyo yule Yoshua mkuu alivyomweka Mungu kwanza, akawaweka makuhani na sanduku la agano kwanza.”

¹⁶⁶ Hilo ni somo halisi, laiti tungalikuwa na wakati wa kulitafakari kwa muda kidogo. Mtangulize Mungu kama unataka kuona jambo fulani. Kama daktari alikwambia amefanya yote awezayo kukufanyia, mtu huyo ni mwaminifu, basi kama amefanya yote awezayo kufanya, mweke Mungu huko nje sasa. Mweke Mungu huko na umwache huko. Mchukue Mungu kuwa Mponya wako, uone kile atakachofanya.

¹⁶⁷ Daktari ana kikomo, Mungu hana kikomo. Daktari anaweza kufanya chochote. . . Anaweza—anaweza kufanya kazi kwa hisi mbili: kile anachoweza kuona, na kile anachoweza kugusa, ndizo mbili pekee kati ya hisi zake zitakazotangaza chochote. Mungu, jamani, Yeye—Yeye—Yeye ni rasilimali ambazo hazijatumika, Yeye ana vitu vyote, anaweza tu kunena Neno, na litakuwa hivyo. Mweke Yeye kwanza.

¹⁶⁸ “Ndipo wakaenda Yordani, Yordani ikafunguka.”

¹⁶⁹ Naye akawazia, “Unajua, jiwe lenyewe ninalokalia sasa, nguvu za Mungu zilitikisa upande wa juu wa ule ukuta, zikaubomoa, jiwe lenyewe ninalokalia, nguvu za Mungu zilitikisa zikalitoa ukutani pale, kwa watu kupiga makelele na kumsifu Mungu, kuta za Yeriko zikaanguka chini kabisa, moja juu ya lingine.” Kupaza sauti kidogo husaidia mara moja moja, naamini, hakika husaidia. “Nayo. . . Ndipo walipopiga tarumbeta, hao watu wakapiga makelele, kuta zikaporomoka. Na kuwazia ya kwamba ninii hasa. . .”

¹⁷⁰ Je, unasema, “Vema, laiti ningalienda kule na kuketi juu ya moja la mawe hayo?”

¹⁷¹ Kiti chenyeve unachokalia ni Neno la Mungu lililodhihirishwa; dunia yenyewe unayotembelea ni Neno la Mungu lililodhihirishwa; mavumbi ardhini ni Neno la Mungu. Amina. Loo, jamani! Jengo hili ni Neno la Mungu, dawati hili ni Neno la Mungu, Mungu aliliumba, aliliumba kwa Neno Lake Mwenyewe.

¹⁷² Hakukuwa na kitu cha kulifanyizia, Yeye alisema, “Na iwe,” Naye akaliadini Neno Lake Mwenyewe, na kulikuwako na ulimwengu uliotokea. Loo, jamani! Niko tayari kufunga nafsi yangu kwenye sehemu Yake yoyote, na kusema ni kweli. Naam, bwana. Yeye alisema, “Na iwe,” ikawa, kwa sababu Yeye ni Mungu, Yeye alifanya Neno Lake Mwenyewe kutimia. Angali anatimiza Neno Lake Mwenyewe, daima alilitimiza, na daima atafanya hivyo. Atasimama na Neno Lake, anayoahidi Mungu, Mungu atafanyia.

¹⁷³ Ibrahimu alikaa katika nchi ya kigeni miaka ishirini na mitano, akizeeka wakati wote, sabini na mitano kabla Mungu hajamwita. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁷⁴ Ungeweza kuwazia mwanamume mzee na mwanamke kama huyo wakishuka kwenda ofisini mwa daktari, na kusema,

“Vema, Dak, tunataka kufanya maandalizi na hospitali, tutapata mtoto?”

Angesema, “Maskini jamaa mzee, yuna kasoro.”

¹⁷⁵ Hivyo ndivyo kila mwaminio wa kweli wa Mungu anavyofikiriwa. “Naam, nafikiri kuna kasoro . . .” Kuna kasoro, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani; umeyapita mambo ya ulimwengu ukayaamini mambo ya Mungu.

¹⁷⁶ Mkristo huangalia yasiyoonekana, si yale anayoona, anaangalia yale asiyookana. *Huoni* kwa macho yako, kwa vyovyote vile, *unaona* kwa moyo wako. Hiyo ni kweli. Unaangalia kwa macho yako, *unaona* kwa moyo wako. Ni kweli.

¹⁷⁷ Huninii . . . Unaelewa. *Kuona* ni “kuelewa.” Unakiangalia kitu hicho moja kwa moja, na kusema, “Sikioni.” Unamaanisha hukielewi; hilo ndilo neno lake halisi.

¹⁷⁸ Sasa, ndipo Ibrahimu, akatoka, na kusema, “Sara, tutapata mtoto. Ninawatakeni mwende sasa, nasi tutanunua jicho-ndege na pini, na kushona vijibuti vidogo, tujiandae.”

¹⁷⁹ Mwezi wa kwanza ukapita: “Ibrahimu, hakuna tofauti.” Mnaona, alikuwa amekoma hedhi muda mrefu wakati huo. Kasema, “Hakuna tofauti.”

¹⁸⁰ Mwezi wa pili ukapita: “Hakuna tofauti, Ibrahimu. Kama tu vile ilivyokuwa.”

“Haleluya! Tutampata mtoto, kwa vyovyote vile.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha.”

¹⁸¹ Mwaka mmoja ukapita: “Kuna tofauti yoyote, Sara?”

“La, hakuna tofauti.”

¹⁸² “Utukufu kwa Mungu! Tutakuwa na . . . Itakuwa ni mwujiza mkubwa zaidi kuliko ilivyokuwa kama ingetendeka mwaka uliopita. Mwaka mmoja zaidi sasa, mimi nina umri wa miaka sabini na sita nawe una sitini na sita. Haleluya! Mwujiza mkubwa kuliko vile ungalikuwa kama tungalikuwa wadogo kwa mwaka mmoja. Hakuna tofauti bado?”

“Hakuna tofauti.”

¹⁸³ Miaka kumi ikapita: “Bado hakuna tofauti.”

“Mungu asifiwe, tutampata, kwa vyovyote vile.”

¹⁸⁴ Ati nasi tunapaswa kuwa wana na binti za Ibrahimu, ati hao ni watoto wa Ibrahimu, na lisipotukia katika dakika mbili baada ya kuombewa, tunasema, “Loo, sikulipata.” Loo, wewe hustahili kuitwa mwana na binti ya Ibrahimu namna hiyo.

¹⁸⁵ Ibrahimu, na badala ya yeye kudhoofika, Biblia ilisema alipata nguvu zaidi wakati wote, akapata nguvu zaidi. Alipokuwa na umri wa miaka mia moja, bado alikuwa akimsifu

Mungu. alikuwa anaenda kumpata, naye akampata. Walikuwa na mtoto huyu, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

¹⁸⁶ Mungu anapaswa kuaminiwa kwa Neno Lake. Yale asemayo Mungu hutimia, haidhuru ni ya muda gani, ni nini, Mungu alisema hivyo, naye unalishikilia tu. Hivyo tu. Kaa tu nalo, litakuvusha.

¹⁸⁷ Kulikuwako na Bartimayo ameketi pale, aliwazia, “Loo, kama jiwe lili hili linaloning’inia ukutani, na nguvu za Mungu kwa watu kupiga makelele, lilianguka kutoka ukutani, ni jambo la ajabu jinsi gani!” hapana shaka aliwazia. “Hilo lilikuwa ni jambo zuri sana. Loo, laiti ningaliishi wakati Yoshua alipovuka ile Yordani, ningekimbia kule kwa Yoshua, na kusema, ‘Yoshua, ewe shujaa mkuu wa Mungu, ninajua ya kwamba wewe ni mtu wa Mungu, Mungu amekuita, wewe ni—wewe ni mtu mashuhuri. Omba kwa ajili ya macho yangu yaliyopofuka, Yoshua. Nami na—najua nitaona kama tu utaniombea.”

¹⁸⁸ Lakini ole wangu, “Siku za miujiza zimepita,” kanisa lake lilisema. “Hatuna huo tena. Mungu haponyi tena, Yeye hafanyi miujiza, Yeye ni Mungu tu. Anatutarajia tuwe makasisi wazuri sana, na kuwa na elimu nzuri, na kujua jinsi ya kuzungumza na watu, na kusema ‘Amina,’ vizuri sana, nanyi mnajua, na mambo kama hayo, na—na mambo ya kiakili.”

¹⁸⁹ Hilo lina jambo lile lile leo, halijabadilika hata kidogo. Mwajua, she—shetani humchukua mtu wake, bali kamwe si roho yake; naye Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si roho Yake. Kwa hiyo wangali wanapigana ndani ya wanadamu vile vile tu. Mmoja atasema . . . loo, wa kidini sana, kama Esau na Yakobo na kadhalika, mwajua, wa kidini sana, lakini hata hivyo hawaamini mambo ya kimbinguni. Lakini ya kimbinguni yanapokuja, hubadilisha mambo. Mungu huja miongoni mwa watu Mwenyewe na kujionyesha Mwenyewe ya kwamba Yeye ni Mungu, ya kwamba Yeye ni Yehova.

¹⁹⁰ “Halafu Yoshua, baada ya kuja upande huu, siku moja alikuwa akitembea huku na huku akiangalia zile kuta, akiona jinsi zilivyokuwa nene na jinsi zilivyokuwa kuu, akitembea huku na huku, naye akamwona Mtu. Ndipo huyo Mtu akauchomoa upanga, akaanza kumwendea Yoshua. Naye Yoshua akauchomoa upanga wake, akaanza kumkabili huyo Mtu, Yoshua akasema, ‘Je, Wewe uko upande wetu? Wewe ni wa adui yetu?’

¹⁹¹ “Naye yule Mtu aliyekuwa na upanga uliochomolewa, akasema, ‘La, mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana.’

¹⁹² “Yule shujaa Yoshua akauangusha upanga wake, akatupa chapeo yake, akailaza chini ngao yake, akainama miguuni pa huyo Mtu, Amiri wa jeshi la Bwana.” Loo, jamani! “Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana.”

¹⁹³ Bartimayo kipofu hapana shaka alisema hivi: “Loo, wazia, Mtu huyo alisimama si zaidi ya yadi mia moja kutoka mahali

ninapoketi. Laiti ningaliishi tu wakati huo, ningalimkimbilia huyo Amiri wa jeshi la Bwana, na kusema, 'Ee Amiri Mkuu wa jeshi la Bwana, nifungulie macho yangu tena nipate kuona ili nipate riziki kwa ajili ya familia yangu.' Naye huyo Amiri wa jeshi la Bwana angeyafungua macho yangu. Lakini ole wangu, walisema siku za miujiza zimepita."

¹⁹⁴ Hakujua hata kidogo, hakujua hata kidogo, ya kwamba chini ya yadi mia moja alisimama Amiri yuyo huyo, akija tena katika Jina la Bwana njiani Mwake.

¹⁹⁵ Hivyo ndivyo ninavyowazia sasa, watu hawa kwenye vitanda, na kwenye viti, na wenye ugonjwa wa moyo, na chochote mlichio nacho, na kansa, Amiri yeye yule wa jeshi la Bwana yuko papa hapa, usiku wa leo, katika umbo la Roho Mtakatifu. Laiti ungalifungua macho yako na kuangalia, ufahamu wako, upate kujua ya kwamba Yeye yuko miongoni mwetu.

¹⁹⁶ Angalia, muda si muda mwajua, alisikia kelele ikija. Mnajua kuna kitu cha ajabu, kila mahali unapomwona Yesu, daima unapata kelele nyingi, sijui ni kwa nini ilikuwa hivyo. Wala haijabadilika kamwe, ungali unapata kelele nyingi sana mahali alipo.

¹⁹⁷ Wakati mmoja walijaribu kuwafanya watulie, Akasema, "Wakinyamaza, hayo mawe yatapiga kelele mara moja." Kitu fulani kukihusu ambacho kina kelele.

¹⁹⁸ Naye akasikia kelele zikija, na baadhi yao walikuwa wakiimba, "Hosana, hosana kwake Yeye ajaye katika Jina la Bwana!" Hao wengine walikuwa wakidhihaki, wakifanya mzaha. Hao wakatoka nje ya lango.

¹⁹⁹ Huyu hapa anakuja kijana Mwanamume katika miaka Yake ya thelathini, akitembea amekielekeza kichwa Chake Yerusalemu, mizigo ya ulimwengu, dhambi zote za ulimwengu zikiwa juu Yake. Huyu alikuwa ni Amiri wa jeshi la Bwana, huyo alikuwa Ndiye aliyekuwa pamoja na Yoshua kule nyika-... ama, pamoja na Musa nyikani, huyo alikuwa Ndiye yeye yule aliyekuwa pamoja na Elisha kule nyuma aliyemfufua yule mtoto mchanga; Amiri yeye yule aliyekuwa pamoja na Yoshua, Amiri yeye yule aliye hapa usiku wa leo, Yule yule atakayekuwa Bwana Mungu yeye yule milele na milele, Yeye habadiliki, Amiri jeshi yule yule wa jeshi la Bwana.

²⁰⁰ Naye huyu hapa akitembea. Nami ninaweza kusikia watu wikipiga makelele, "Aisee, wewe! Hebu tukuone ukifanya mwujiza. Hebu tukuone ukifanya mwujiza, tunataka kuuona, tunasikia ati unafanya miujiza." Unapowasikia watu wakisema hivyo, unajua wana roho ya namna gani, ni ibilisi.

²⁰¹ Angalia kile Yesu, alipoona...wakati ninii...Shetani alipompeleka nyikani, alisema, "*Ikiwa* wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate. Una njaa, nawe unataka chakula, kwa hiyo yafanye tu mawe haya mkate kama wewe

ni Mwana wa Mungu, itanifanya nikuamini, kama tu utafanya hivyo.”

²⁰² Yesu hamjali ibilisi; hakuna mtumishi wa Mungu anayemjali ibilisi. Yesu alisema, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate pekee.’”

²⁰³ Walipompeleka kwenye—kwenye nyua za Kirumi katika nyua za mahakama ya Kirumi, walimfunga kitambaa usoni na kuchukua fimbo na kumpiga kichwani, kasema, “Sasa, wanasema wewe ni nabii, kwamba unaweza kusema mambo ambayo ni... yale watu wamefanya, na yale watu watafanya, sasa tuambie ni nani aliyekupiga, tutakuamini.”

²⁰⁴ Angeweza kufanya hivyo, bali angekuwa akimjali ibilisi. Hakufanya hivyo, aliketi tu pale wala kamwe hakufungua kinywa Chake. Akiwa amefungwa kitambaa usoni Mwake, wakampiga, akasema, “Wewe ni nabii, uh? Tuambie ni nani aliyekupiga sasa, tutakuamini.”

²⁰⁵ Ibilisi yuyo huyo anaishi ndani ya watu siku hizi. Asema, “Kama wewe ni... Kama kuna Mungu, Mponyaji... Kama jamaa huyu ana karama ya uponyaji wa Kiungu, ashuke aende, akamponye huyu *hapa*, hebu nione, nitaamini. Hebu nione.” Mwajua, makanisa hueneza propaganda ya namna hiyo. Kumbukeni tu, hiyo ni roho, roho ile ile.

²⁰⁶ Hao makuhani wakasema, “Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, shuka utoke msalabani sasa, ifungue mikono yako ushuke chini, na—nasi tutakuamini.” Mbona, angalifanya hivyo kama angalitaka kufanya hivyo.

²⁰⁷ Mnajua, walimpa heshima kuu sana hapo aliyowahi kumpa, Kayafa, yule Kuhani Mkuu, hao walisema, “Aliwaokoa wengine, mwenyewe hawezi kujiokoa.” Hiyo ilikuwa ni heshima. Kama Yeye aliwaokoa wengine, Yeye—Yeye asingeweza... Kama alijiokoa Mwenyewe, asingeweza kuwaokoa wengine, kwa hiyo alijitoa Mwenyewe kusudi aweze kuwaokoa wengine. Mnaona? Ilimbidi kujitoa ili aweze kutuokoa sisi. Kama angalijiokoa Mwenyewe... .

²⁰⁸ Kama vile Billy Sunday alivyosema, moja ya maandishi yake, kimoja cha vitabu vyake nilichokuwa nikisoma hapa siku moja, kilisema, “Malaika walikuwa wameketi katika kila mti, wakisema, ‘Vuta tu mkono Wako kutoka msalabani uuelekeze kwa mmoja wetu, tutabadilisha mandhari hii hapa.’”

²⁰⁹ Angeweza kufanya hivyo, pia, lakini kama angalifanya hivyo, tungekuwa wapi leo? Lakini Yeye aliangikwa pale amejaa mate usoni Mwake, na misumari mikononi Mwake, na miiba kichwani Mwake, na Damu ikitiririka na machozi yaliyochanganyikana, akifa kama mhalifu kwa sababu Yeye alitupenda. Hiyo ni kweli. Na kutupa nafasi kwa ajili ya wokovu, akitupa nafasi ya kuwaombea wagonjwa, nao wangeponywa, akitupa nafasi hiyo, aliyofanya kwa ajili yake.

²¹⁰ Na huyu hapa yule Amiri wa jeshi la Bwana akitoka. Ninaweza kumsikia kasisi yuyo huyo ambaye ndiyo kwanza aongee naye muda mfupi uliopita, na kusema, “Simile. Hatutaki yoyote ya ibada hizo za uponyaji mjini mwetu, kundi la watu lililochochewa kabisa, na kadhalika namna hiyo, kwenye kundi la ushupavu wa dini, nabii fulani kutoka Galilaya aliyezaliwa mwana haramu. Wala kamwe hakuenda kwenye seminari yetu, hajui lolote kuhusu shule zetu, kamwe hakuwa mshiriki wa dhehebu letu, hatujui lolote kumhusu. Tutakomesha tu kitu hicho, hatutakuwa na uhusiano wowote nacho, nina hakika ya hilo.”

²¹¹ Tunamsikia kasisi yuyo huyo akisema, “Hei! Tunasikia ya kwamba ulimfufua mtu jina lake Lazaro, tuna uwanja mzima wa makaburi uliojaa hao hapa juu, njoo ukamfufue mmoja wao. Njoo huku juu kando ya kilima, tumekuwa tukiwazika huko juu kwa mamia ya miaka, njoo huku juu ukamfufue mmoja wao, tutakuamini.”

²¹² Lakini mnajua nini? Hakuzingatia hilo hata kidogo. Alikuwa akienda Zake Yerusalemu kutolewa kama Dhabihu, mzigo wote wa ulimwengu juu ya Nafsi Yake ya thamani. Alikuwa akielekea Yerusalemu, akipanda moja kwa moja mlimani wakati huo kwenda Yerusalemu kusulubiwa, kwa ajili ya watu wale wale waliokuwa wakimdhahiki. Walikuwa wakimtupia tunda au mayai yaliyooza, wakimdhahiki, wakimfukuza kutoka mjini. Lakini hakulijali hata kidogo, aliendelea tu kusonga mbele.

²¹³ Bartimayo alishtuka, akasema, “Haya yote yahahusu nini? Kuna nini? Vurugu hizi zote ninazosikia ni za nini?”

Ndipo mtu fulani akasema, “Simile, ombaomba.” Wengine *hivi, na vile*.

²¹⁴ Ndipo hatimaye, ninaamini hapana shaka ilikuwa ni mama fulani wa thamani, jamaa huyo mzee alikuwa amesukumwa kutoka kwenye huo mwamba, naye akasema. . . yeye akasema, “Umeumia, bwana?”

“La, mama, sijaumia, lakini siwezi kuelewa, kelele hizi zote ni za nini?”

“Mbona,” akasema, “Yesu wa Nazareti, Nabii wa Galilaya, anapitia njia hii.”

“Mwanamke wangu mwema. . .”

²¹⁵ Hapana shaka alikuwa mfuasi wa Yesu, maana wafuasi wa Yesu sikuzote wanajali, nao ni wema na wanapenda kuwasaidia watu, wanapenda kufanya jambo fulani kumsaidia mtu fulani, wafuasi wote wa Yesu wanatenda hivyo. Kama ni wazee wanaojaribu kuvuka barabara, mfuasi wa Yesu hapitii tu hapo karibu na kuwaacha wasimame hapo wapate kukanyagwa, yeye husimama na kuwasaidia kuvuka barabara; na wakimwona maskini mzee mwenye lundo kubwa la vyakula,

mfuasi wa Yesu anawasaidia kuvipeleka nyumbani; na—na wakiona mhitaji, wanaenda kuwasaidia, hivyo ndivyo wafuasi wa Yesu wafanyavyo. Daima ni wema, wenye moyo mwororo, wakionyesha huruma, wakitenda mambo kwa mtu fulani.

²¹⁶ Ndipo huyu mfuasi wa Yesu akasema, “Mbona, bwana, hivi huwafahamu manabii?”

“Vema,” akasema, “nilikuwa tu nimeketi hapa kidogo nikiota juu ya yale manabii waliyozoea...yale mama yangu alikuwa akiniambia kuhusu manabii.”

“Vema basi,” akasema, “Huna budi kufahamu ya kwamba Masihi yuaa.”

²¹⁷ “Loo, naam, naam. Tunajua ya kwamba Masihi atakuja, kwa sababu Musa alisema Bwana, Mungu wetu, atamwinua Nabii aliye kama yeye. Na kila mtu asiyemsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali na watu. Atakuwa Nabii mkuu atakapokuja.”

²¹⁸ “Vema,” akasema, “bwana, Mtu huyu ndiye huyo Nabii. Mbona, Yeye huwaangalia watu, huyatambua mawazo yao, anawaambia jambo hasa lililo moyoni mwao, Yeye huwaambia mambo ambayo wamefanya, mambo yatakayotukia, na kila wakati ni kamilifu.”

“Loo, unamaanisha kwamba Mtu huyu amewasili?”

“Huyo Ndiye anayepita.”

“Vema, kwa nini watu wanapiga makelele namna hiyo, na kupayukapayuka, na kumdhihaki?”

²¹⁹ “Kwa sababu hawamjui. Lakini sisi tunamjua Yeye, kwa sababu sisi ni waaminio, tunamjua Yeye, tunamfuata Yeye kila siku. Tunaangalia na kuona miujiza anayofanya, nasi tumeshawishika ya kwamba huyu ni—huyu ndiye Masihi. Mbona, nilimwona, hapa wakati fulani uliopita, wakati alipokuwa akizungumza na yule mwanamke kisimani, Akasema, ‘Nenda kamwite mumeo.’

“Naye akasema, ‘Sina mume.’

“Akasema, ‘Umesema vema. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.’

²²⁰ “‘Mbona,’ akamwambia, ‘Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.’ Mbona, Yeye...yeye alisema, ‘Mimi...Tunajua, sisi Wasamaria tunajua Masihi ajapo, Yeye atatuambia mambo haya.’

“Naye Mtu huyu akasema, ‘Mimi ninayesema nawe Ndiye.’

²²¹ “Ndipo akakimbia mjini, akisema, ‘Njoni, mwone Mtu ambaye ameniambia yale niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?’ Basi mji wote wa Samaria ukaongoka.”

“Usiniambie! Vema, kama Yeye ndiye Masihi, huyo ni Mwana wa Daudi.”

“Naam, hiyo ni kweli, Huyo ni Mwana wa Daudi.”

Naye akapaza sauti, “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!”

²²² Ndoto yake inaweza kutimia sasa. Labda yako ingeweza, dada kwenye kitanda cha wagonjwa, ndoto yako ya afya tena ingeweza kutimia. Yako, kwenye kiti cha magurudumu, yako, uliyeliwa na kansa, ndoto yako ya kurudi kanisani na kufanya upya nadhiri zako na Mungu, labda ndoto yako iko karibu tu kutimia. Labda Amiri huyo wa jeshi la Bwana anapita baada ya kitambo kidogo, ninatumaini ya kwamba anapita.

²²³ “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu!” Loo, asingeweza kumsikia kimwili, Alikuwa huko nje barabarani, na mamia ya watu wakikusanyika pande zote, mmoja akipiga mayowe jambo moja na mwingine lingine. Ndipo akatupa nyuma koti lake lililochakaa, na kupaza sauti, “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Nirehemu!”

²²⁴ Hebu na tuchukue tu jambo dogo ambalo ninaamini alilifanya, sijui kwamba alilifanya, ninaweza kuwazia alisema moyoni mwake, “Ikiwa huyo ni Mwana wa Daudi, basi ninaweza kusimama papa hapa na kumwomba Yehova, Yehova atasema Naye.” Hiyo ni kweli. “Yehova anaweza kumsimamisha, maana Yeye anajua hali yangu. Nami nimekuwa nimeketi hapa nikitamani kumwona.”

²²⁵ Mnajua, hiyo ndiyo njia ya kumleta Mungu karibu nawe, ni kuwazia juu Yake, kuzungumza juu Yake. Mweke tu Yesu... Usiongee mambo ya ulimwengu, nena habari za Yesu. Hiyo ndiyo njia ya kufanya hilo. Watu huenda wakafikiri wewe ni wa ajabuajabu kidogo, lakini hilo ni sawa, endelea tu, acha mazungumzo yako yawe kumhusu Yeye.

²²⁶ Hapa, nataka kusimama hapa kwa dakika moja. Mwanangu, Billy, yuko hapa mahali fulani, hapa yapata miaka mitatu ama minne iliyopita, tulikuwa mkutanoni, naye... walikuwa wakicheza muziki wa namna fulani, ama kitu fulani, tulienda baada ya ibada huko Wood River, Illinois, nasi tukaenda kununua cha—chakula, nao walikuwa wakicheza namna fulani ya wimbo, sijui ulikuwa ni upi.

Naye akasema, “Baba, huo si ni wimbo mzuri?”

Nikasema, “Wimbo gani?”

²²⁷ Nami ninayadharau maskini hayo masanduku ya santuri, chochote mnachoyaita. Nimeingia kwenye mikahawa mingi, nikasema, “Mama, nitaweka dola mbili hapa chini, nina familia yangu, kama utazima kitu hicho kichafu hapo, mpaka familia yangu imalize kula. Wewe kizime tu.”

²²⁸ Maskini hizo roki, na bugi-bugi, na kadhalika, ni fedheha, zinanifanya niwe na wasiwasi sana, huwezi kula. Mimi—mimi—mimi mwenyewe sikijali, maana nina gia ndogo ninayoweza

kujiingiza, ninaendelea tu kuwazia juu ya Mungu, wala sikisikii hata kidogo.

²²⁹ Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, alikuwa mseja wakati huo, kabla hajaoa, maskini msichana fulani angepita karibu, naye akasema, “Baba, hivi si ana nywele nzuri?”

Nikasema, “Nani?”

Akasema, “Baba, yote unayowazia ni Biblia na Mungu.”

²³⁰ Nikasema, “Asante, Mpenzi, hiyo ni sifa nzuri sana. Hilo tu ndilo ninalotaka kuwazia.” Hiyo ni kweli. Wazia... Kama ninaweza tu kuweka nia yangu imetulia Kwake wakati wote, hilo tu ndilo linalohitajika.

²³¹ Hapo, alisimama pale, naye akawaza, “Nilikuwa nikimwazia, naye Huyu hapa karibu nami sasa. Lakini kuna wengi kupita kiasi kati yangu na Yeye, si—si—sijui nitakalofanya. Ee Yehova Mungu, huyo ni Mtumishi Wako, huyo ni Mwanao. Wewe ulisema, ya kwamba ‘Mtumishi Wangu, ambaye ninapendezwa Naye. Nitaweka Roho Yangu juu Yake, Yeye atawaonyesha Mataifa hukumu,’ na kadhalika. Huyu ni Mtumishi Wako. Ee Mungu, loo, jalia Yesu wa Nazareti, jalia aseme nami.”

²³² Yapata wakati huo, Yeye akasimama. Loo, jamani! Akasimama, akageuka. Hakumsikia kimwili, alikuwa mbali sana naye. Kama umewahi kuwa huko Yeriko, angalia mahali... pale... mahali lilipotukia. Katika umati huo wote, Yeye asingeweza kumsikia, kwa vyovyote vile. Lakini huninii... Si lazima akusikie, imani yako ndiyo inayomsimamisha.

²³³ Mwangalieni maskini yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, akipitia kwenye ule umati, naye akasema, “Loo, laiti ningaliweza tu kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Naye akajipenyeza, mpaka akagusa upindo wa vazi Lake.

²³⁴ Sasa, vazi la Kipalestina linapwaya, ni joho, nalo lina vazi la ndani. Sasa, kamwe nisingekuhisi wewe kama ungegusa mfuko wangu, kimwili. Ni zaidi sana vipi joho kubwa, linalopwaya? Hakumhisi kimwili kamwe, kwa kuwa Yeye—Yeye alisema, “Ni nani aliyenigusa?” Naye akaangalia pande zote.

Ndipo Petro akamkemea, kasema, “Vema, kila mtu anakugusa. Kwa nini useme jambo kama hilo?”

Akasema, “Lakini naona kwamba nguvu zimenitoka.”

²³⁵ Ndipo akaangalia kote, kisha akaangalia kwenye kusanyiko, ndipo akamwona maskini mwanamke huyo huko nje kwenye kusanyiko. Naye akasema alikuwa ametokwa na damu, na imani yake ilikuwa imemwoko.

²³⁶ Sasa, Mungu yuyo huyo kule chini, alijua... Alipokuwa Yesu yeye yule akipaa juu, Bartimayo kipofu asingeweza kumfikia, alikuwa mbali sana Naye, bali imani yake ikamsimamisha Yesu.

Tazama, Yeye alizibeba dhambi za ulimwengu. Alikuwa na ma—mauti ya kila kiumbe kilichowahi kufa, ama kitakachopata kufa, yamewekwa juu Yake; alikuwa na kila dhambi iliyowahi kutendwa, ama itakayopata kutendwa, imewekwa juu Yake; naye alikuwa akienda Zake Kalvari, katikati ya makundi ya watu wa dini waliopiga mayowe wakimdhahiki, na kumpa changamoto awafufue wafu ama kumponya mtu fulani, lakini imani ya ombaomba huyo kipofu bado ilimsimamisha akienda zake.

²³⁷ Ninataka kuhubiri usiku mmoja, nikiweza, juu ya *Yesu Akasimama Kimya*, nione ni mara ngapi lilitukia.

²³⁸ Wakati Yesu aliposimama kimya pale, na kugeuka, alisema, “Mleteni hapa. Ungetaka nifanye nini?”

Loo, ninaweza kumwona. Wakati umegundua kwamba umepata usikivu Wake!

“Loo,” kasema, “tazama, Yeye anakuita, uwe na moyo wa ushujaa.”

²³⁹ Akatupa koti lake, mwangalieni, hakuliweka vizuri sana apate kujua angelipata atakaporudi, mahali ambapo angeweza kulipata, alijua kama akipata kukutana na Yesu, angeweza kuona koti lake atakaporudi. Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, hiyo ndiyo njia. Kama angewahi kuja na kufanya mahojiano na Yesu, ingekuwa tofauti, ndipo angeweza kuona tangu wakati huo na kuendelea, kwa hiyo akatupa tu koti lake. Akaenda zake!

Naye akasema, “Ungetaka, nikufanyie nini?”

Akasema, “Bwana, nipate kuona.”

²⁴⁰ Hilo ndilo lililokuwa niani mwake, hakuzungumza Naye jinsi Mbinguni kulivyokuwa kuzuri. Bali alikuwa na haja, “Nataka nifunguliwe macho. Niweze kuona.”

²⁴¹ Yesu akasema, “Upate kuona, imani yako imekuokoa,” ile imani iliyomsimamisha. Na kama imani yetu usiku wa leo inaweza kumsimamisha, kama imani yetu usiku wa leo inaweza kumleta hapa chini, tunaweza kupokea uponyaji wetu, kile tunachohitaji.

²⁴² Hadithi ndogo kabla ya kufunga. Nilisoma hadithi ndogo ya kubuni, hapana shaka ilikuwa ni hekaya, ilidhaniwa kuwa ni kweli, lakini nina shaka nayo, kuhusu Bartimayo. Nilikuwa nikiyachukua maisha ya manabii, na kadhalika, nami nikasoma makala juu ya Bartimayo.

²⁴³ Walisema alikuwa kipofu tangu alipokuwa m—mvulana. Nanyi mwajua, katika siku hizo, siku hizi mtu anapokuwa kipofu, ninasahau wale mbwa wanaowaongoza wanaitwaje, mwajua, na, namna fulani ya mbwa anayemwongoza kipofu, mbwa wa jicho lionalo, katika siku hizo, badala ya kuwa na mbwa, walikuwa na mwana-kondoo aliyeongoza. Naye

Bartimayo alikuwa na mwana-kondoo, naye alikuwa na njiwa wawili wadogo.

²⁴⁴ Nayo ikasema kwamba usiku mmoja alikuwa na, alikuwa na binti mdogo, maskini binti mdogo, mwenye nywele za shaba, ndipo usiku mmoja, maskini huyo msichana akawa mgonjwa, naye alikuwa... alienda akaomba, naye akasema, “Bwana, kama utamjalia msichana wangu mdogo kupona, nitakutolea Wewe njiwa wangu, kesho.”

²⁴⁵ Hilo lilikuwa ndilo jambo pekee... Maskini hao njiwa walifanya vitimbi pamoja, na hayo mazingaombwe madogo ya kuvutia usikivu wa watalii, nao wangemrushia kitu fulani kwa ninii yake... sarafu katika kikombe chake.

²⁴⁶ Basi akasema, “Bwana, kama utanijalia tu nipone, nitawapeleka njiwa wangu wawili kanisani kesho, nami nitakutolea sadaka hawa njiwa wawili.” Ndipo homa ya maskini huyo msichana ikaisha, akapona.

²⁴⁷ Majuma machache baada ya hapo, mkewe akashikwa na ugonjwa, naye tabibu akasema hakuna kitu angaliweza kufanyiwa, alikuwa amefanya yote aliyojua. Naye akatoka nje ya jengo, akipapasa-papasa kando ya nyumba. Naye akasema, “Loo, Yehova, kama utamjalia mke wangu mpendwa kuishi, nitakuahidi, sina kitu kingine cha kukupa, kwa hiyo nitakupa mwana-kondoo wangu,” yule aliyemwongoza kule juu.

²⁴⁸ Na kwa hiyo kesho yake asubuhi, mke wake akapata nafuu, kwa hiyo akaenda zake, kumpeleka mwana-kondoo wake akatolewe dhabihu. Walisema alikutana na kuhani mkuu, akasema, “Bartimayo kipofu, unaenda wapi asubuhi ya leo?”

²⁴⁹ Akasema, “Loo, kuhani mkuu wa Mungu, ninaenda hekaluni kumtoa dhabihu mwana-kondoo wangu. Mke wangu alipona nilipomwomba, nami nilimwahidi Yehova ningempa mwana-kondoo huyu.”

²⁵⁰ Ndipo kuhani mkuu akasema, akaingiza mkono kwenye mfuko wake wa fedha, na kusema, “Loo, Bartimayo, huwezi kumtoa huyo—huyo mwana-kondoo.” Kasema, “Nitakupa pesa, nawe uende kwa—kwa wanunuzi, ama wabadilishaji,” kisha kasema, “nenda kule ukajinunulie mwana-kondoo wa sadaka.”

²⁵¹ Akasema, “Loo, kuhani mkuu, nakushukuru sana, lakini,” kasema, “Kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo *fulani*, nilimwahidi mwana-kondoo *huyu*.”

²⁵² Hiyo ndiyo shida kubwa sana siku hizi, rafiki. Pasaka, tunajaza madhabahu yungiyungi. Mungu... Madhabahu haikufanywa kwa ajili ya yungiyungi, madhabahu ilifanywa kwa ajili *yako*, unaona. Unaona? Lakini sisi—sisi tunataka kuleta kitu kingine kuchukua mahali petu, hatuwezi kufanya hivyo, Kibadala chetu tayari kimeletwa, Kristo.

²⁵³ Akasema, “Kamwe sikumwahidi mwana-kondoo fulani, nilimwahidi mwana-kondoo huyu.”

Naye kuhani mkuu akasema, “Bartimayo, huwezi kumtoa mwana-kondoo huyo, mwana-kondoo huyo ndiye macho yako, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo.”

Akasema, “Loo, kuhani mkuu wa Mungu, hakika hiyo ni kweli, lakini kama nitatimiza ahadi yangu kwa Mungu, Mungu atatoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.”

²⁵⁴ Ilikuwa ni asubuhi hiyo baridi ambayo yule Mwana-kondoo ambaye Mungu alikuwa amemwandaa, yule Mwana-kondoo wa Mungu aliyekuwa ametolewa kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu. Ninaweza kumwona baada ya Yeye kusema, “Upate kuona,” amesimama, katika dakika chache, akaiangalia mikono yake. “Loo, Yeye aliniambia ningepata, alisema macho yangu yangeona.” Umati ulikuwa ukishuka barabarani. Baada ya kitambo kidogo, aliona kivuli, akasema, “Loo, hiki hapa! Ninaanza kuona vidole vyangu vikisogea.” Huyu akaenda, akimtukuza Mungu. Hakika. Mungu alikuwa ametoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.

²⁵⁵ Mwana-kondoo yuyo huyo ametolewa kwa ajili yako, dada, kwa ajili yako, dada, kwa ajili yako, kwa ajili yako, kwa ajili yangu, kwa yeyote atakaye, Mungu anaye Mwana-kondoo aliyetolewa kwa ajili yetu usiku wa leo kwa ajili ya macho yetu, kwa ajili ya macho yetu, kusudi macho yetu ya kiroho yafunguke, na kutambua ya kwamba ni Bwana Yesu Kristo katikati yetu. Na atuajalie usiku wa leo, ndilo ombi langu.

²⁵⁶ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya hadithi hizi za Biblia, ni muhimu sana kwetu, tunazipenda, kwa sababu ni uzima kwetu. Tunaona kile ulichokuwa, na kile ulichokuwa jana, ndivyo ulivyo leo, na utakuwa milele.

²⁵⁷ Sasa, Mungu Mtakatifu, Muumba wa Mbingu na nchi, mtume tena, usiku wa leo, Roho Mtakatifu. Yesu alisema, “Roho Mtakatifu atakapokuja, atayachukua mambo haya yaliyo Yangu na kuwaonyesha. Atawaonyesha mambo yajayo, atashuhudia kweli. Yeye atanishuhudia Mimi,” alisema Yesu. Nasi tunajua ya kwamba ni kweli.

²⁵⁸ Nami naomba, Baba, ya kwamba usiku wa leo ya kwamba Roho Mtakatifu atafanya zile kazi hapa katika hili kusanyiko ambazo Yesu alifanya alipokuwa hapa duniani, wapate kufahamu, nayo macho ya watu hawa yangefunguka, kila mmoja wao. Wengi wao ni Wakristo wazuri, waaminifu, nao wanakupenda, na wanakupenda kwa mioyo yao yote.

²⁵⁹ Sasa, Baba, yafungue macho yao ya kiroho, wapate kufahamu, ya kwamba mambo haya ni yale hasa uliyosema yangetukia, ni ahadi Yako hasa, yale uliyotuahidi. Na jalia tuuone usiku wa leo, mkono wa Mungu aliye hai miongoni

mwetu. Ndipo macho ya watu wote yatafumbuliwa, na ndipo sisi sote tutapokea uponyaji wetu, wokovu wetu, na ninii. . .

²⁶⁰ Kanisa litakapofungwa usiku wa leo, jalia twende nyumbani kama wale waliotoka Emau, baada ya Wewe kufa, na kuzikwa, na kufufuka tena, ukatembea pamoja nao siku nzima, nao hawakukutambua, lakini ulipojifungia ndani pamoja nao, peke yenu, jioni hiyo, ulifanya jambo fulani kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa, wakatambua ya kwamba Wewe hukuwa mfu tena, ya kwamba ulikuwa umefufuka katika wafu, kwa kuwa hakuna mtu angaliweza kufanya mambo hayo jinsi Wewe ulivyoyafanya, nao wakakimbia, wakishangilia, wakisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?”

²⁶¹ Jalia jambo lile lile lirudie usiku wa leo. Bwana, njoo miongoni mwetu, uchukue miili yetu, uchukue maskini mwili wangu huu, kama unaweza kuutumia, fanya hivyo. Baba, huwezi kutumia wangu bila kutumia yao, kwa hiyo tumia mwili wa wagonjwa, tumia nafsi zetu na miili yetu usiku wa leo kwa heshima na utukufu Wako, ili wengine wapate kuona na kuponywa. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, Amiri wa jeshi la Bwana. Amina.

²⁶² Kama kulikuwa na njia inayowezezana kwangu kufanya uponyaji, kama ningeweza kumfanya mama huyu hapa ainuke kutoka kwenye kitanda hiki cha wagonjwa anacholalia na kuondoka, ni—ni—ningechukua robo na kuisukuma kwa pua yangu kuzunguka mji huu, kuliona likitendeka. Mimi. . . Vipi kama mimi. . . Vipi kama huyo. . . Vipi kama ilikuwa ni dada ya—yangu, mama yangu, mke wangu aliyelala pale? Vipi kama huyu alikuwa mmoja wa ninii yangu. . . Vipi kama wewe huko nje uliye na kansa, au ugonjwa wa moyo, vipi kama ilikuwa ni mama yangu, ndugu yangu, mwanangu, binti yangu? Jamani! Lakini, laiti ningaliweza, lakini siwezi.

²⁶³ Na kama Yesu angesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, wala Yeye asingeweza, tayari amefanya hivyo. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba wokovu na kila baraka ya ukombozi tayari imenunuliwa? Basi angefanya nini kama angalikuwa hapa? Yeye angetenda tu kama alivyofanya alipokuwa hapa duniani, afanye jambo ambalo ungeona ya kwamba Yeye alikuwa ni Yesu aliye hai.

²⁶⁴ Sasa, ni wangapi wanajua jambo hili? Kwamba Yesu alisema ya kwamba katika wakati huu wa mwisho, tumekuwa tukihubiri juu yake juma hili, kwamba Roho wa Mungu angekuja duniani, anayeitwa Roho Mtakatifu, na angefanya kazi zile zile alizofanya. Ni wangapi wanaojua hilo? Aonyeshe ishara ile ile aliyoonyesha, aliwaonyesha Wayahudi, akawaonyesha Wasamaria, bali Yeye kamwe hakuwaonyesha Mataifa, haikuwa ni siku yao. Wala Mataifa hawakuwa wakimtazamia Masihi.

Lakini leo hii tunakutazamia Kuja kwa pili kwa Kristo. Sasa, hatuna budi kupokea ishara ya Masihi, ambayo ndiyo ishara ya mwisho.

²⁶⁵ Basi kumbukeni, mnakumbuka Yeye alinena juu ya Nuhu? Lakini hakusema wakati huo, bali alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Yeye alizungumzia yale maadili ya—ya siku za Nuhu, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, lakini “kama vile siku za Sodoma,” Yeye aliacha hilo. Mnaona? Hilo ni ufunuo.

²⁶⁶ Waangalie wale Malaika, jinsi tumekuwa tukizungumza juu ya yale waliyofanya. Zile huduma, mwangalieni Billy Graham siku hizi, vile vile hasa, Oral Roberts wa kisasa, Billy Graham, hao wainjilisti mashuhuri wanaozunguka ulimwenguni, wakiita kutoka Babeli, kutoka Sodoma, kila wawezacho. Je, inakuwa bora zaidi? Mbaya zaidi wakati wote.

²⁶⁷ Sasa angalieni lile Kanisa teule. Mnaamini katika uteuzi? Hakika itabidi iwapo mnaamini Biblia. Majina yetu yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, inasema Biblia. Mnaona? Tuliteuliwa na Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye alituchagua.

²⁶⁸ Sasa, sasa, na halafu, kama tumeitwa, unapaswa kumshukuru Mungu kwamba uliteuliwa, hilo ndilo ninaloshukuru sana juu yake, kwamba Mungu aliniita, akanichagua. Sikumchagua kamwe, Yeye alinichagua. Hukumchagua kamwe, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo unaona, Mungu akikuita, Yeye atabisha mlangoni pako, huo ndio wakati wako wa kuja.

²⁶⁹ Sasa, leo ni siku ya Mataifa. Hii ndiyo siku, Ujumbe wa mwisho... Basi kumbukeni, Sodoma ilianganimizwa, hapo Moto uliposhuka kutoka Mbinguni.

²⁷⁰ Je, ninyi nyote mmekuwa mkisoma gazeti juu ya mkutano huu wa hadhara unaoendelea hapa California, jinsi watu hao wanavyozungumza kuhusu kuhama kutoka chama kimoja hadi kingine? Lakini bila shaka, kwangu mimi, mi—mimi, nilipiga kura moja, hiyo ilikuwa ni ya Yesu Kristo kama Mwokozi wangu, nitashinda. Hiyo ni kweli. Hilo ni sawa. Nilimpigia kura Bwana Yesu kuwa Mwokozi wangu, na ni hivyo tu. Mnaona? Sasa, ninaamini katika kupiga kura, ninaamini unapaswa kufanya hivyo, lakini mimbara hii si mahali pa kuzungumzia hilo, zungumzieni hayo popote mtakapo, hii ni Injili hapa, hii ni kitu ninachojua ni kinyofu, na safi, na ni kweli, nami ninajua itatukia, hivyo tu.

²⁷¹ Sasa, wakati Yeye akiwa hapa, wakati Yesu anapokuja kwetu usiku wa leo, ninawatakeni mkumbuke ya kwamba kila baraka

ya ukombozi ambayo Yeye angeweza kuwapa, “A—*alijeruhiwa* kwa makosa yetu, *alichubuliwa* kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*.” Kila mtu aliokolewa, kila mtu aliponywa wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, bali huna budi kuwa na imani yako binafsi Kwake upate kuokolewa au kuponywa.

²⁷² Sasa, kama Yesu angekuwa hapa usiku wa leo, ungesema, “Bwana Yesu, shuka, uweke mikono Yako juu yangu,” na kukuponya.

²⁷³ Unajua kile Yeye angesema? “Mwanangu, hivi huliadini Neno Langu? Unaadini Neno Langu? *Nilijeruhiwa* kwa makosa yako, kwa kupigwa Kwangu wewe *uliponywa*.”

²⁷⁴ Sasa, Neno Lake linapaswa kutosha, lakini basi... Kama hamkuliadini neno langu, labda ningeliachilia tu; kama sikuamini lako, ungeniachilia, bali si Mungu, kama huamini Neno Lake, basi bado Yeye alimtuma Roho Mtakatifu pamoja na karama Kanisani. Ya kwanza ni ipi? Mitume, manabii, wainjilisti, waalimu, wachungaji, yote kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa, Kanisa lipate kumjua Yeye. Mwalimu, mchungaji, mwinjilisti, nabii, mambo haya yote ni ya kuninii—ni ya kufanya ijulikane... .

²⁷⁵ Ni Wapentekoste wangapi walioko hapa usiku wa leo? Vema, ninyi watu mnaadini katika kunena kwa lugha. Paulo alisema, “Kama kuna mmoja miongoni mwenu sasa anayenena kwa lugha, wala hakuna anayefasiri, isipokuwa iwe ni kwa ajili ya kujenga, mtu fulani wa kuifasiri, isipokuwa iwe ni kwa ajili ya kulijenga kanisa, mbona, watu wajinga wataingia, waondoke na kusema, ‘Mbona, nyote mna kichaa, nyote mmeingia wazimu.’” (Ambalo *wazimu* linamaanisha “kichaa.”) “Na kusema, ‘Mbona, nyote ni wendawazimu.’ Lakini kama mmoja ni nabii, naye atatoa unabii na kufunua hilo jambo, basi itawabidi hao kuanguka chini na kusema, ‘Hakika, Mungu yu pamoja nanyi.’” Kwa sababu hiyo ndiyo ishara ya mwisho ya Mungu. Tunajua jambo hilo, na jambo ndilo hilo, tunaliishia leo hii. Bwana awabariki.

²⁷⁶ Sasa, nilisahau... Yuko wapi Billy Paul? Yeye...? Samahani. Yeye ni mdogo sana, siwezi kumwona. Uligawa kadi ngapi? Hamsini? Ulianzia hamsini, ama...? Moja hadi hamsini, sawa.

²⁷⁷ Hatuwezi kuwaweka wote mstarini mara moja, kwa hiyo hebu tuwapange tu kadiri tuwezavyo. Vema, kadi ya maombi namba moja, ni nani aliye nayo? Ni herufi gani? B? B, namba moja? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁷⁸ ...kuwa halisi, la sivyo mimi ni nabii wa uongo na mdanganyifu, na Biblia imekosea. Mungu wa Ukristo aliahidi ya kwamba angekutana hapa, “Popote mtakapokusanyika, nitakuwa pamoja nanyi.”

279 Alimtuma Malaika na kuniambia, “Usiogope. Nime... Umetumwa kuwaombea wagonjwa, utajua siri yenyewe ya moyo wao.” Mimi...

280 Sasa, maono yalianza kuja... Jambo la kwanza ninaloweza kukumbuka maishani lilikuwa ni ono, daima imekuwa hivyo. Umezaliwa na karama hizi, hamwekeaneni mikono ninyi kwa ninyi kwa ajili ya karama za namna hii, karama hizi, Mungu huweka kanisani. Hiyo ni kweli, ndugu? Mnaona? Mungu huziweka kanisani, unazaliwa nazo, ni za asili, za asili tu kama kitu kingine chochote.

281 Sasa, ninatumaini ya kwamba Yeye atatujalia Uwepo Wake. Kama akifanya hivyo, baraka Zake kuu na ziwe juu yetu. Iweni na kicho, aminini.

282 Mnasema, “Kwa nini unasitasita, Ndugu Branham?”

283 Ninamngojea Yeye. Hiyo ni kweli kabisa. Asipokuja, siwezi kufanya lolote, bali kama akinitia mafuta, ninaweza kufanya hivyo.

284 Sasa, angalieni, yeyote yule anayeitengeneza maikrofoni hii—hii hapa, kwa sababu huenda ikawa kwamba mimi... sauti yangu wakati mwingine... Haijulikani, hujui unalosema. Ni ono, unaona jambo fulani likitukia, na, mahali pengine. Kwa hiyo sasa, kama ikitokea haina sauti kubwa vya kutosha, waambieni baadhi ya hao watu.

285 Kumbukeni, ninyi nyote, tuonane kesho usiku Bwana akipenda. Mungu awabariki. Sasa, Bwana Yesu na abariki tunapimba kwa upole *Amini Tu*, kila mmoja wetu pamoja sasa.

Amini tu...

286 Ninaweza kumwona wakati akishuka kutoka kilimani, mtoto mwenye kifafa pale. Akasema, “Bwana, mrehemu mtoto wangu, amepagawa sana na pepo.”

Yesu akasema, “Ninaweza, kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana, amini tu.”

Mambo yote yanawezekana, amini tu.

287 Ninachukua kila roho humu ndani chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa, huyu—huyu ndiye mtu huyo? Je, huyu ni mmoja wa watu wa kuombewa?

288 U hali gani, bwana? Sasa, tunakutana, nadhani, kwa mara yetu ya kwanza maishani. Hiyo ni kweli? Vema. Sisi ni wanadamu wawili tu wanaokutana. Sikujui, nawe hunijui. Na labda uko hapa kwa ajili ya ugonjwa fulani, au mpendwa fulani, au suala la kifedha, sijui unachoninii... matatizo ya kinyumbani, chochote kile, Mungu anajua yote kuyahusu.

289 Sasa, ingeweza kuwa kwamba ningetembea hapa, baada ya kuwaambia mambo haya niliyo nayo, na kuwawekea mikono,

na kusema, “Nitakuombea, ndugu yangu, basi nenda ukawe mzima.” Ama labda huenda nikafanya, kama baadhi ya ndugu zetu wahudumu, kukuwekea tu mikono yetu, na kumkemea huyo pepo, na kadhalika, kama baadhi ya hao ndugu walio na imani halisi, tunayoita, “imani ya ubabe,” kama vile Ndugu Oral Roberts anavyowekea mikono yake juu yake, naye ana imani halisi, na kukihukumu kitu hicho, na namna hiyo. Hiyo—hiyo ni huduma ya Ndugu Roberts. Mnaona?

²⁹⁰ Naye Mungu—Mungu hashughuliki na watu wawili kwa usawa. Siwezi kupachukua mahali pa Ndugu Roberts, wala yeye hawezi kupachukua mahali pangu. Sote wawili tuna huduma, inatubidi kufanya jinsi unavyotuambia tufanye.

²⁹¹ Lakini sasa, kama ningekuja hapa juu, na kusema, “Vema, ndugu—ndugu, nina huduma ya kuwawekea mikono.” Nami ningekwambia hilo, nawe uendele, labda ungepona, hiyo ni kweli. Lakini sasa, ungeweza kushuku hilo kidogo. Unaona? “Sasa, hivi aliniambia ukweli au la?”

²⁹² Sasa, kama Yesu Kristo angali hai kama alivyokuwa katika siku zilizopita, nami ninaweza kujitolea kwa Roho Wake, bila kukujua wewe, basi kama Kitu fulani kikiingia ndani yangu, na kuanza kufunua jambo ambalo ni, jambo ambalo umefanya huko nyuma, kama alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, kama alivyomwambia Simoni Petro alipomjia, na loo, sehemu nyingi sana katika Biblia, mnaona, kama akianza kukwambia kile ulichokuwa, vema, utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli. Ndipo utakuwa shahidi wa hilo, nawe utajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, unaweza kushuhudia kama ni hivyo ama sivyo.

²⁹³ Ndipo kama akikwambia yale yaliyokuwako, kisha akwambie yatakayokuwako, kama kile kilichokuwako ni kweli, basi kile Yeye anachokwambia hakika kitakuwa ni kweli. Hiyo ni kweli, enyi wasikilizaji? Mnaona? Basi haikubidi kubahatisha. Huyu ni Roho wa Bwana.

²⁹⁴ Sasa, sisemi ya kwamba atafanya hivyo, ninatumaini ya kwamba atafanya hivyo. Lakini kama atafanya hivyo, kusanyiko tayari limeahidi, huyu papa hapa, kama angemwambia huyu mtu, afanye tu jambo lile lile alilofanya wakati Simoni alipomjia, kasema, “Wewe—wewe ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona,” ama kumwambia yeye alikuwa ni nani, ama Filipo, ama baadhi ya hao wengine namna hiyo, ambavyo aliwafanyia walipomjia, mbona, ingemfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, sivyo? Kufanya Uwepo Wake hapa, Amiri Mkuu wa jeshi la Bwana.

²⁹⁵ Sasa, sina fununu ni nini . . . kwangu anaonekana kama mtu mwenye afya, hakuna kitu kumhusu kingeonekana kisicho na afya. Lakini hakika kuna . . . Huenda asiwe mgonjwa, huenda ikawa ni kitu kingine, Bwana anajua. Sasa, Bwana na anisaidie, naomba Roho Mtakatifu wa Mungu aje kwangu, na kunena

kusudi watu wajue, wajue ni Roho fulani, nao watahukumiwa kwa kile wanachomwita.

²⁹⁶ Mungu, Wewe ndiwe Mwamuzi. Jalia iwe, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana, si kwa ajili ya maonyesho, bali kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

²⁹⁷ Sasa, kama watu wangali wanaweza kuisikia sauti yangu, mtu huyo ananiondokea. Ana shida, shida yake iko kwenye fuvu lake la kichwa, kichwani mwake. Yeye . . . Hapo ndipo shida yake ilipo. Ni . . . ? Hiyo ni kweli, sivyo, bwana? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

²⁹⁸ Sasa, kuna—kuna nguvu fulani zinazojua hilo kumhusu mtu huyo, mimi sijui. Unasema . . . Huenda kukawa na ninii mpya . . . Kuna mtu yeyote hapa, hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo kabla? Inua mkono wako. Hajawahi kamwe kuwa mkutanoni hapo kabla. Huenda mkafikiri nilibahatisha. Vema, hebu tuone. Hebu Yeye . . .

²⁹⁹ Sijui ilikuwa ni nini, kanda pale zinayo; hiyo ndiyo sababu tunaweka kanda hizi, kila kitu kilichosemwa. Hakuna jambo moja lililowahi kusemwa, pasipo Bwana kuthibitisha kwamba ni kweli.

³⁰⁰ Naam, hili hapa: huyu mtu anaugua kitu fulani kichwani mwake. Ni ninii . . . aliumia. Ilikuwa kitu fulani kuhusu magogo, ama kitu fulani kuhusu ustawi wa magogo, ama kitu fulani, BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

³⁰¹ Hutoki hapa, umekuja hapa kwenye mkutano huu, umetoka California. Hiyo ni kweli. Unafikiri Mungu anajua wewe ni nani? Angeweza kuniambia wewe ni nani? Ingekusaidia? Utaamini ingekufanya . . . ? Ungefanya hivyo? Vema, Bw. Robinson, unaweza kurudi nyumbani na uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya.

³⁰² Unamwamini Bwana? Sasa, mnaona, angalieni marafiki, huyo si mimi. Mimi, Mungu anajua, siwezi kuwaambia jambo moja aliloambiwa mtu huyo, ni ono, ninaangalia yale yanayotukia. Mnaona? Sasa, hilo ni jambo lile lile . . . Ni wangapi humu ndani, waaminio, wanaojua ya kwamba hilo ni jambo lile lile alilofanya Yesu Kristo alipokuwa hapa duniani, na akaahidi ya kwamba ingekuwa ni ishara ya wakati wa mwisho? Sasa, tunaweza kusema nini zaidi? Yeye yupo hapa, sasa wewe mwamini Yeye. Hilo linapaswa kulitatua, kusanyiko lote linapaswa kusimama na kusema, “Asante Bwana, aliniponya,” unaendelea. Hiyo ni kweli. Yote yamekwisha, Yeye amelithibitisha.

³⁰³ U hali gani . . . ? Je, hii ni . . . ? Sijarukwa na akili, bali maono, inakubidi kuangalia. Wewe—wewe ni . . . Unaona, ninakuangalia hapa, kisha ninakuona mahali fulani, unajua ninalomaanisha, ono. Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi

Wake? Unaamini hilo? Hatufahamiani, sikujui, bali Mungu anakujua.

³⁰⁴ Sasa, hii ni picha nyingine nzuri kama Yohana Mtakatifu 4, ninyi wasomaji wa Biblia, mwanamume na mwanamke walikutana kwa mara yao ya kwanza maishani, mwanamke wa Samaria na Yesu wa Nazareti. Mnakumbuka hadithi hiyo? Yesu alifanya nini? Alikuwa na haja ya kupitia Samaria, Mungu alimtuma huko juu; Nilikuwa na haja ya kuja kwenye Maporomoko ya Klamath, Mungu alinituma huku.

³⁰⁵ Mwanamke alikuja na alikuwa akizungumza na Yesu. Yesu alizungumza naye muda mrefu kutosha kuwasiliana na roho yake, naye akapata shida yake ilikuwa nini na kumwambia, ndipo akasema, “Hapana shaka Wewe ni nabii. Tunajua kwamba ajapo Masihi,” ambaye ni Bwana Yesu, “Masihi, atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya.”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

³⁰⁶ Sasa, kama—kama uliwahi kuwa Samaria, ni kisima, kimefanya mandhari ndogo, kama hii tu hapa. Hii hapa hapa hadithi ya namna fulani ikirudiwa tena. Huyu hapo, simjui, nasi hatufahamiani na tunakutana hapa kwa mara ya kwanza. Sijui mwanamke huyo amesimama hapo kwa sababu gani, bali Mungu anajua kilichomleta hapa, Yeye anajua yote kuhusu hilo.

³⁰⁷ Kama Mungu atanifunulia jambo ambalo ndilo shida yako, shida *fulani* tu, ama—ama chochote kilichokuleta hapa, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake?

³⁰⁸ Kusanyiko litafanya vivyo hivyo? Huyu mwingine alikuwa ni mwanamume, hebu wanawake wote waamini.

³⁰⁹ Sasa, huyu mama anajua, sasa hivi, ya kwamba jambo fulani linaendelea. Kati yangu na huyo mwanamke inasimama ile Nuru. Ni wangapi wameiona kwenye picha? Je, mna...? Picha zote ziko hapa. Gene, nyote mnaleta hizo picha jukwaani? Unapaswa kuchukua moja. Ni picha iliyo na hatimiliki, imetundikwa kwenye Ukumbi wa Sanaa wa Kidini huko Washington, DC, Ndicho Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha kisayansi; hiyo ni kwa serikali. Kilipigwa picha hapa (Ni mahali gani hapa tunapoelekea hapa, California?), Lakeport.

³¹⁰ Una matatizo fulani, moyo, matatizo mbalimbali ambayo unaugua. Hutoki hapa, kutoka kwenye mji huu. Unatoka kwenye mji mwingine, unaoitwa Lake-fulani, Lakeview, ndiko unakotoka. Hiyo ni kweli. Unamjali mtu mwingine unayemwomba, pia. Ana shida ya rektamu pia, ni kitu kama—kama bawasiri, ila tu zaidi sana ni kama uvimbe. Una kitu puani, pia, kinachokusumbua, puani mwako. Hiyo ni kweli.

³¹¹ Unaye binti hapa. Hiyo ni kweli. Namna fulani ya ugonjwa kama wa ngozi, shida ya miguu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli,

sivyo? Mume wako asingeweza kuja, lakini yeye ni mgonjwa, pia. Unaamini ninaweza kukwambia kwa Roho Mtakatifu shida yake ni nini? Bawasiri. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ingekusaidia? Waweza kwenda nyumbani na kuamini yale niliyokwambia kuwa ni kweli? Ungefanya hivyo, kwa vyovyote vile. Vema, Bibi Trachsel, unaweza kwenda nyumbani basi ukaponywe, Yesu Kristo alikuponya. Mungu akubariki, dada.

³¹² Unamwamini Bwana Yesu? Hilo linapaswa kulitatua kwa kusanyiko.

³¹³ U hali gani, bwana? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote, unaninii... Wewe ni mtu mzuri sana, unasimama hapa kwa ajili ya mtu mwingine, ana uvimbe. Hiyo ni kweli. Nenda ukaamini sasa, naye atapona. Amina.

Mwamini tu Mungu, usiwe na shaka.

³¹⁴ Huyu mama aliyeketi moja kwa moja huko nyuma, yeye ni mama wa watoto wadogo, wagonjwa. Uligusa Kitu fulani wakati huo, mama. Uliamini, sivyo? Wewe mwenyewe una bawasiri unayotaka iombewe, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Watoto wako wadogo ni wagonjwa, una seti mbili za mapacha. Hiyo ni kweli, sivyo mama? Hiyo ni kweli, inua mkono wako.

³¹⁵ Aligusa nini? Angalieni mahali anapoketi. Alifanya nini? Kamwe hakunigusa, alimigusa Yeye, Kuhani Mkuu, Akageuka.

Usijali, mama, umeponywa, nao watoto wako watakuwa wazima. Imani yako inakuokoa, kama unaweza kuamini.

³¹⁶ Huyu hapa mama ameketi huku ameinamisha macho yake namna *hiyo*, alikuwa akijiombea, ana yabisi kavu. Unaamini Bwana atakuponya, dada, uliyeketi hapo? Ulikuwa unaomba, ukasema, “Bwana, jalia aniite.” Hiyo ni kweli, inua mkono wako kama hivyo ndivyo ulivyosema katika maombi yako. Ninajuaje yale uliyosema katika maombi yako?

Mwamini Mungu, usiwe na shaka.

³¹⁷ U hali gani, bwana? Hatufahamiani, sikujui wewe, na—na, lakini Mungu anakujua. Kama Bwana atanifunulia jambo fulani kukuhusu, utamwamini kwa moyo wako wote? Ungefanya hivyo. Shida yako iko katika, kichwani mwako. Una ugonjwa wa kichwa chako. Una kifafa, kidogo unazirai, na kadhalika. Una shaka kidogo kuhusu wokovu wako, pia, huna hakika kabisa kama uko sawa kabisa au la, hiyo ni kweli.

³¹⁸ Na kinachosababisha jambo hili, ulipata ajali iliyolisababisha, ndivyo ilivyo. Bw. Woodland, unaamini ya kwamba hiyo ni kweli? Hilo ndilo lililohitajika, sivyo? Vema, endelea, utakuwa sawa. Mungu akubariki.

³¹⁹ Kuwa tu na imani, amini kwa moyo wako wote. Mungu atakujalia haja yako kama tu utamwamini. Je, wewe...?

Kuamini? Sasa angalia, unajua ya kwamba kitu fulani hakina budi kufanya hivyo. Hiyo ni kweli? Sasa, ni Roho wa namna gani? Unaamini Huyo kuwa ni Roho wa Mungu?

³²⁰ Sasa, Mafarisayo walimwambia Yesu ya kwamba Yeye alikuwa Beelzebuli alipofanya hivyo. Akasema, “Ninawasamehe kwa kusema hivyo, lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja ukisema neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe.” Hiyo ni kweli? Sasa, waulizeni baadhi ya watu hawa ambao wamefanyiwa huo mwujiza, waulizeni, mwone kama ni halisi. Mungu anajua ya kwamba ni halisi *sana*.

³²¹ U hali gani, mama? Mtu anayeonekana mwema. Angalia tu, unaona jinsi inavyokuweka? Unakuwa tu dhaifu sana, kusanyiko lote linaonekana kana kwamba linaogelea pande zote, pande zote kwangu. Kumbukeni, Yesu aliona ono moja, mtu mmoja alimgusa, Naye akasema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka.” *Nguvu* ni nini? Ni uweza.

³²² Baadhi yenu huko nje sasa, ambao hamna kadi za maombi, na kadhalika, ombeni, wewe huko nje, mwangalie Mungu, na kusema, “Mungu, ninakuamini. Mtu huyu hanijui. Laiti ungenigusa, Ee Bwana Mungu, laiti ungenipa afya, acha tu aseme nami, nitaamini kwa moyo wangu wote.”

³²³ Ninatoa changamoto kwa imani yenu kwa hilo. Msiniamini, mwamini Yeye, maana mimi ni mwanadamu tu, kama tu maikrofoni hii. Si maikrofoni mnayoisikia, ni sauti yangu; si mimi mnayenisikia, ni Yeye.

³²⁴ Bwana, unayeketi hapo na ugonjwa wako wa mgongo, unaamini ya kwamba Yesu Kristo atakuponya, akupe afya? Mke wako ameketi karibu nawe hapo, ana shida ya vidole vyake. Unaamini Mungu atamponya, pia? Wewe dada, unaamini, pia? Hilo lilikushtusha, sivyo, ndugu? Hukujua ulikuwa na imani kiasi hicho. Weka mikono yako juu ya mke wako, ana namna fulani ya kitu kama maambukizi, yanamsumbua mikononi mwake, wekeaneni mikono sasa.

³²⁵ Shetani, ninakukemea, toka ndani ya watu hawa!

³²⁶ Katika Jina la Yesu Kristo, jalia waponywe. Amina.

³²⁷ Sasa, kwenu ninyi wawili mliloitwa sasa hivi, hivi kuna mmoja wenu asiye na kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi? Huhitaji moja. Vema. Sasa, ulikuwa na nini? Ulikuwa na imani. Ulimgusa nanii Mkuu... Sikujui, kama hiyo ni kweli, inua mikono yako, kama hatufahamiani. Wala sijawahi kukuona maishani mwangu, nadhani hujawahi kuniona. Lakini imani hiyo kidogo haikujulikana kwako, bali uligusa Kitu fulani, Naye akakupa thawabu kwa kwa ajili yake, sasa utakuwa mzima. Usijali, imani yako imekuponya.

³²⁸ Kama huyo si Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, sijui Biblia. Naam, bwana. Ni kweli.

329 Samahani, mama. Ninaninii tu, angalia, ni zamu yako ya kuombewa, nilikuwa tu nikiliangalia kusanyiko, kusudi watu waone ya kwamba ha—haihitaji ka—kadi ya maombi kuwaponya watu, mnaona, i—i—inahitaji imani katika Mungu. Hiyo ni kweli. Inahitaji imani katika Mungu kuwaponya watu. Kama utakuwa tu na imani na usiwe na shaka, Mungu atakuponya.

330 Unaonaje juu ya jambo hilo, Bw. Robison, uliyeketi hapo ukiwa na henia? Unafikiri ya kwamba Mungu angekuponya? Unaamini? Vema, bwana.

331 Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu, sijawahi kumwona maishani mwangu, bali alikuwa ameketi pale akiwazia hilo.

332 Hiyo ni kweli, sivyo, bwana? Inua mkono wako. Unaona, Yesu alijua yote kuhusu yale unayoombea na yote kuyahusu.

333 Amini tu. Kama utaamini kwa moyo wako wote kwamba yanatoka kwa Mungu, hata shida yako iwe nini, itakwisha. Alikupenda vya kutosha kukuita; unapomwita, Yeye anakujibu. Yeye si ni wa ajabu?

334 Unaugua maumivu makali ya kichwa wakati wote, uliyeketi moja kwa moja hapo nyuma mwishoni. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama unaamini, siku za kuumwa na kichwa zimekwisha.

335 Hatufahamiani, sikujuu. Huenda tumeachana kwa miaka kadhaa, na—na maili nyingi, na—na hapa tunakutana. Lakini Yesu anatumia sote wawili, hiyo ni kweli. Kama Yeye, kwa nguvu Zake kuu, atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo unajua kwamba silijui, itakupa tu msaada mkubwa? Ingekupa.

336 Jaribu hili mara moja, moja zaidi. Angalia—angalia kama Roho wetu Mtakatifu... Mtu mwema namna hiyo akingojea wakati huo wote. Ndipo tutakuwa na maombi kwa ajili ya watu wengine.

337 Wewe kweli upo hapa kwa niaba ya mtu mwingine, upo hapa kwa ajili ya mtu aliye na wasiwasi, wasiwasi wa akili, hali, kwa namna fulani wanarukwa na akili. Hiyo ni kweli. Nawe umeweka lesa hapa juu kumpelekea mtu huyo. Hiyo ni kweli. Hutoki kwenye mji huu, unatoka mahali panapoitwa Grants Pass, juu ya Mto Rogue. Hiyo ni kweli.

338 Una namna fulani ya ugonjwa wa moyo, magonjwa ya ziada. Hiyo ni kweli. Una binti hapa usiku wa leo, unayemjali, yeye ni binti aliyeasiliwa, kwa kweli yuko mstarini apate ku—kuninii, mstarini kuombewa huko nyuma. Ana moyo ulio na baridi yabisi, uvimbe, koo.

339 Ulikuwa huku kwa basi, utarudi kesho, huu utakuwa usiku wako wa mwisho hapa. Hiyo ni kweli. Aisee, umekuwa mhudumu, mhubiri mwanamke, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI, hiyo ni kweli. Sasa unaamini? Basi nenda nyumbani na upokee

yale hasa uliyoomba, na Mungu wa Mbinguni akubariki daima. Ingia tu ndani, dada, i—imekwisha, utakuwa mzima. Kamwe usi—usitie shaka, endelea tu, amini.

³⁴⁰ Sasa, nisingeweza kumwona huyo msichana kutoka mahali mwanamke huyo alipokuwa amesimama, bali nilimwona hapa nje mbele yangu. Sasa, mnaamini, ninyi nyote, kwa nia moja? Mnamwamini Bwana Yesu, kila mmoja? “Kila atakaye, na aje.”

³⁴¹ Bwana, kama utamwamini Mungu, hiyo yabisi kavu itakuacha. Unaamini hilo? Basi nenda zako na kushangilia, na kusema, “Asante, Bwana, kwa kuwa mwema sana kwangu.”

³⁴² Nawe una jambo lile lile. Jambo lingine la mtu wa umri wako kweli angekuwa na tezi dume, nyeusi kidogo inayokufanya uwe na wasiwasi, na kadhalika. Kama utaamini kwa moyo wako wote, unaamini? Basi nenda zako, na kusema, “Asante, Bwana, nitakuwa mzima.” Vema, bwana.

³⁴³ Wewe ni kijana mwanamke mwenye ugonjwa wa moyo, lakini unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo? Nenda zako, na useme, “Asante, Bwana Yesu, kwa kuniponya.”

³⁴⁴ Vema, njoo, mama. Umetiwa uvuli, kuna kivuli cheusi kinachokufuata, ambacho kinamaanisha kwamba una kansa, kimetiwa uvuli wa mauti. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya na kukupa afya? Inua mkono wako, useme, “Ninaukubali, Bwana.” Nenda zako, upate afya. Amini kwa moyo wako wote.

³⁴⁵ Njoo, mama, tafadhali. Vema, una ugonjwa wa mgongo. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuuponya mgongo wako? Nenda zako ukapate afya. Amini kwa moyo wako wote.

Mnaamini huko nje?

Vema, njoo, bwana. Una ugonjwa wa pumu. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuuponya? Nenda zako, na useme, “Asante, Bwana,” uponywe.

Njoo, bwana. Una kisukari. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya kisukari? Nenda zako ukapate afya. Amini kwa ninii. . . shida zako zote.

Shida yako iko mgongoni mwako, ulijeruhiwa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Nenda zako ukaponywe, na umwamini Mungu.

Njoo, bwana, upande huu. Hebu kidogo, naona mtu huyu ana roho kiziwi. Inamisha kichwa chako kwa dakika moja tu.

³⁴⁶ Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa kila karama njema, yafungue masikio ya mtu huyu na kumfanya asikie, Bwana. Hawezi kusikia, na imani chanzo chake ni kusikia, hii roho kiziwi juu yake. Yafungue, Bwana, ninaomba katika Jina la Yesu.

347 Shetani, mwachilie!

348 Umekuwa hivi kwa muda gani? Muda mrefu? Unaweza kunisikia vizuri sasa? Vema. Unanisikia sasa? [Ndugu huyo anasema, “Loo, ninakusikia waziwazi, lakini maneno hayatengani. . . ? . . .”—Mh.] Unanisikia sasa? Unasema, “Amina.” “Nampenda Bwana.” “Bwana asifiwe.” Yanatengana vizuri sasa. Umeponywa. Jambo lingine, uliponywa wakati mmoja hapo awali katika mikutano yangu. Amina. Niliona wakati ilipotukia. Amina. Mungu. . . Mungu alikuponya miaka mingi iliyopita. Mungu akubariki.

349 Yeye si ni wa ajabu? Je, Bwana wetu si ni wa ajabu? Sasa, niambieni jambo moja ambalo Yeye hafanyi.

350 Sababu ya kumpeleka mtu huyo pale kwa ajili ya jambo hilo, sijui alikuwa ni kiziwi jinsi gani. Alisema viwambo vya masikio yake vilipasuliwa kwa fataki ya baruti. Na kwa hiyo, sikujua kama angeweza kusikia lolote ama la, nilijua tu kwamba alikuwa na uziwi. Na hiyo ndiyo sababu. . . Kama hawezi—kama hawezi kusikia, vema basi, nilipoenda kumwombea, nilimwona amesimama kwenye mstari mwingine, kisha nikaona Utukufu wa Mungu juu yake. Naye aliponywa katika mkutano mwingine, na kwa hiyo mtu huyo ni mzima sasa, mzima kabisa. Hiyo ndiyo sababu unamshikilia namna hiyo, na kumshikilia mpaka itendeke, mpaka aweze kusikia. Halafu imani, anaweza kusikia, imani chanzo chake ni kusikia.

351 Nyote mnamwamini Bwana Yesu? Ni wangapi hapa wanaoamini sasa, na wana hakika ya kwamba Amiri Mkuu, Amiri wa jeshi la Bwana yuko humu jengoni? Mnaamini hilo?

352 Sasa, wekeaneni mikono, hebu tufanye maombi ya kusanyiko. Kila mmoja wenu, kama mnaamini ya kwamba “ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa, hatuwezi kuponya, bali aminini, tafadhali aminini. Anapitia huku.

353 “Yesu, Ewe Mwana wa Mungu, unirehemu! Ewe Mwana wa Mungu, unirehemu!” Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa kila karama njema, tuma baraka Zako juu ya watu hawa ninaowabariki katika Jina Lako.

354 Bwana, mimi ni dhaifu sana, siwezi kusimama hapa zaidi. Ninaomba ya kwamba Roho Wako atakuja katika nguvu kuu na upako, na kulishika kusanyiko hili. Jalia watu wasimame kwa miguu yao wakipaza sauti, “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu!” Ee Mungu, tujalie. Na jalia kila mtu humu ndani aponywe.

355 Shetani, ninakuhukumu juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo, katika mateso ya uwakilishi, ufufuo, toka kwenye kusanyiko hili, waache watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo! 

60-0713 Bartimayo Kipofu
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org